

LILE SHTAKA

 Asante, Ndugu Neville. Hebu tuendeleo kusimama kwa muda mfupi sasa ili tuombe. Na tuinamishe vichwa vyetu. Je, kuna hitaji la kunenwa, ikiwa laweza kujulikana kwa mkono ulioinuliwa? Kwa Mungu tu, sema, Mi—mimi. . . Shikilia mawazoni mwako sasa kile—kile utakacho kumwuliza, na ukiamini kwa moyo wako wote, hali ninapokuombea pia.

² Baba aliye Mbinguni, tuna—hesabu hii kuwa ni heshima kuja kwa nyumba ya Bwana siku hii yenye ukungu, na—na kupata nuru ya Mungu iking'aa, na kusikia Roho Mtakatifu akiimba kupitia kwa watu, na akinena kupitia kwa watu, kama fu—fungu ndogo la nuru ndani. Twakushukuru kwa hili, nuru ya kimbinguni inayozunguka mioyo yetu. Twashukuru vipi kwa ajili hiyo.

³ Sasa, wako—watu wako wameinua mikono yao katika makutano haya, kuwa wana mahitaji ambayo wangetaka uyatimize asubuhi hii. Nami naomba, Baba kuwa utatimizia kila mmoja mahitaki yake. Kunayo mengi sana yaliyokusanywa hapa mezani, na mahitaji mengi kila mahali. Watu wagonjwa, wanaougua; wito wa simu, toka mbali. Karibu hamsini kila siku. Ee, Mungu, tutafanyaje? Tuongoze tu, Bwana. Sisi—hatujui twendee njia ipi wala tutende nini, lakini Wewe—Wewe waweza kuongoza mambo haya. Nasi twaomba kuwa utatupa sisi, kwa sababu ni—ni kusudi letu, Bwana. . . Ni uhai jinsi gani tulio nao duniani tuliopewa nawe, nasi twataka kuutumia kukuheshimu Wewe nao. Sasa utuongoze katika mambo hayo, Baba.

⁴ Tubariki leo hali tumekusanyika pamoja kusikia Neno la Bwana, kuimba nyimbo, kuomba. Sikia maombi yetu. Furahi pamoja nasi katika nyimbo zetu, na nena nasi kupitia kwa Neno, kwa kuwa twaomba katika Jina la Yesu. Amina. Ketini. Sijui mahali popote ambapo ningeona ni heshima kuu kusimama, kuliko vile ingekuwa kusimama mimbarani kuumega ule Mkate wa Uzima kwa watu wanautarajia, wenye njaa na kiu. Na hii ni heshima kuu.

⁵ Kwanza, ningependa kuuliza ikiwa—ikiwa yeyote wa jamaa ya Wright yuko hapa: Hattie, ama Orville, ama yeyote—Hattie. Je, Orville yuko pamoja nawe, Hattie?

⁶ Vema, muulize ikiwa aweza kuja—apitie nyumbani mara moja, kuhusu yale niliyomwambia, wajua, kwa. . . pitia nyumbani ikiwa—akiweza. Nilisahau kukibeba nikilete asubuhi hii, kitu fulani cha mbwa wao mdogo waliye naye pale. Kwa hivyo ni—nina. . . Ukipenda, pitia nyumbani na gari unapokwenda huko—kwa—baada ya ibada.

⁷ Na sasa, Edith, dada ya Hattie, tunayemjua kama msichana mdogo ambaye amekuwa kilema tangu alipokuwa mtoto mchanga, na sasa yeye ni mwanamke sasa; naye yuko katika hali mbaya sana. Sasa ni... Yapata mwaka mmoja uliopita nilikwenda huko alipokuwa mgonjwa kwanza, na mara nilitambua shida yake ilivyokuwa, kwa msaada na neema ya Mungu. Sasa, hakika, shida ya mtoto yule, yeye anaketi—miguu yake imeshikamana na hata hawezi kuitenganisha. Ni kwa ajili ya msongo mwingi kwa—kwa—kwa mishipa ya neva. Lakini jambo ni kwamba, hakuna jambo lo lote baya kwa mtoto yule, ila kuugua kupooza akiwa mchanga, alipokuwa na umri upatao miezi sita. Yeye alipiga mayowe na kulia maishani mwake mwote, karibu mwote, hadi tulipomwombea miaka mingi iliyopita, na—naye amekuwa na furaha tangu wakati huo, hadi yapata mwaka mmoja uliopita. Na sasa, ni kuingia ugumba, yaani, kubadilika kwa maisha yake, na neva zake ziko katika hali baya sana. Na maskini bibi huyo anadhani kuwa anakufa, kuwa yeye, yeye hataishi, saa baada ya saa.

⁸ Nanyi mwajua, wanawake wenye nguvu na afya huwa na shida sana; wakati mwingine inawabidi wadungwe sindano za vitu vilivyo damuni, na—na waende vituoni, na wapate matibabu ya kugutushwa na vinginevyo, wakati huo.

⁹ Mwanadamu ana mabadiliko mawili ya maisha. Wana mabadiliko toka kwa mvulana kuwa mwanamume; toka kwa mwanamke—toka msichana kuwa mwanamke. Wapatapo umri wa miaka kumi na sita, ama kumi na saba wao huanza kuwa kama kundi la wasiotulia. Na—na ukiweza kuwavumilia katika umri huo... Nina binti aliye katika umri huo hivi sasa, Rebeka. Mwombeeni. Na Billy. Jamani, kila mmoja wetu, tumepitia katika wakati huo mfupi wenye kichaa, na—yatubidi tuwastahimili, tukitambua ni kitu fulani ambacho—ambacho wao—wao yawabidi wapitie.

¹⁰ Na sasa, Edith ana badiliko tu la—la miaka saba... Kila miaka saba maisha yako hubadilika, kwa hivyo saba mara saba, mwaona, ni—na ni—inafanya hali kuwa vigumu. Hilo ni badiliko kamili na hu—huwasumbua wanawake. Wanaume kila mara hupata—kutenda yasiyofaa wakati huo na wakati mwingine huwacha wake zao. Lakini wanawake hu—huwa tasa baada ya hayo. Nasi sote twapitia katika hayo. Lazima tukumbuke kuwa ni mambo ambayo lazima tuvumiliane kwayo na tuyaelewa.

¹¹ Na Edith mdogo ana hali hii, naye amepoteza uzito mwingi naye aonekana ana hali mbaya. Na—nawaambia... Usiku mmoja (si ninyi nyote pamoja), lakini kwa safari ndogo tu huko chini... Waliketi pamoja naye mchana na usiku. Na—safari ndogo huko toka Maskani haya na—na Maskani mbali yale—yale Maskani mashirika humu... Baadhi yenu mwende na mwone jamaa ya Wright: nina hakika watafurahia hilo. Nendeni huko, kaeni kwa muda mfupi, na muongee nao,

salimianeni nao kwa mikono, na hata yawe ni matembezi ya kirafiki tu. Sisi—sisi husahau hayo rahisi sana, mwajua. Na iwapo ni nyumbani kwetu, basi tunapendelea hivyo, na lazima tukumbuke wengine pia wanapenda. Na—jamaa ya Wright, nina hakika wangependelea hilo. Ni—najua mngetenda hivyo kama mngalijua kulikuwepo na hali kama hii. Lakini hamkujua, kwa hivyo hapo—basi, nilikuwa nikiwaambia asubuhi hii juu yake.

¹² Nendeni mwatembelee jamaa ya Wright na mjaribu kumfariji Edith. Msimwambie hali yake yaonekana baya, mmwambie aonekana vema. Atapona (naye atakuwa mzima) tukiendelea tu kujipa moyo kwa ajili yake. Tuko hapa kwa ajili hiyo. Yeye ni dada yetu, na—na tuko hapa kujipa moyo katika nyakati hizi kwa ajili ya mtoto huyo; kama tu vile nitakavyo mtu fulani ajipige moyo konde na kuniombea niwapo majaribuni, nanyi mwataka mtu fulani kwa ajili ya yenu.

¹³ Na—na jamaa ya Wright imekuwa—muda mrefu—baadhi ya washiriki wa kale sana wanaokuja kwa kusanyiko hili; wao, na Ndugu Roy Slaughter na Dada Slaughter. Nimewaona tu muda mfupi uliopita, nilipowapungia mkono walipoingia, nikawaza, nilipokuwa nikipiga kona kwa motokaa, “Nimewaona Ndugu na Dada Slaughter kwa miaka mingapi wakiketi mahali pao kanisani humu katika wakati rahisi na mgumu, na bado wangali wanasonga mbele?” Na jamaa ya Wright hivyo... Mwawapenda watu hao. Mwaona? Na hebu hebu tuwaonyeshe upendo wetu kwao.

¹⁴ Na, mimi—leo nina ujumbe mrefu. Unahusu shtaka. Na—tena leo usiku nasikia kuna Meza ya Bwana na kutawadhana miguu, na kadhalika. Kwa hivyo mchungaji atanena, nasi tutakuwa na—tutakuja... Na ikiwa ninyi, mkiwako karibu, njooni na kufurahia—ujumbe toka kwa mchungaji, toka kwa Bwana. Na ndipo pia, toka kwa Kutawadhana Miguu na Meza ya Bwana ya usiku wa leo, utakuwa u—usiku wenye shughuli nyingi sana. Kwa hivyo tutafurahi kuwa nanyi, ikiwa hamna mahali pengine pa kuenda.

¹⁵ Na twataka kuwashukuru Don Ruddell, na—na ndugu yetu, na Ndugu Jackson (na—na ndugu hawa wana—ni ndugu, wa makanisa tunayoshirikiana), Ndugu Jack Palmer hapa, anayesimamia—kundi lile huko Georgia. Nasi—sisi—twataka kuwashukuru watu hawa kwa moyo wetu wote, kwa maana wakati mwingine tukiwa na ibada, nijapo na—wao—huja kututembelea. Nasi twafurahiwa.

¹⁶ Namwona asubuhi ya leo rafiki yangu mwema sana, Dk. Lee Vayle na mkewe. Nilitambua Dada Vayle hapo kwanza, nami nilizidi kutazama alikokuwa Ndugu Lee. Nilipata—(ule msemu wa kale wa Kikusini)—“kunguru wa kudonoa pamoja naye.” Mwaona? Popote nilipopata... Nilimtafuta kila siku mkutanoni, awe hapo anisaidie. Nilisema, “Vema, Lee ajapo, mruhusu

ahubiri, nami nitawaombea tu wagonjwa.” Nasi tulimtafuta, na vinginevyo, hatukumpata; kwa hivyo nina—nina—kunguru wa kudonoa naye nimpatapo . . . Na tuna furaha kuwa na Ndugu na Dada Vayle humu asubuhi hii.

¹⁷ Na labda kunao wengine wengi hapa ambao hatuwafahamu. Namwona dada hapa, naamini atoka Chicago. Siwezi—najua—kundi hapa, lakini siwezi kuwataja majina yao hasa. Basi sisi—twapenda wao toka kokote, popote ulipo.

¹⁸ Naona ndugu hapa, vijana wawili watakaotawazwa (wachanga katika huduma) asubuhi hii. Wawili—ndugu wetu weusi toka huko New York wamepata tu hati zao katika Kanisa la Philidelphia na kusema walitoka kanisa hili. Nasi tutawawekea mikono, ili Mungu abariki huduma zao huko New York. Tunayo huko makanisa mawili au matatu. Naamini Ndugu Milano ana—moja ya hivi vikundi vidogo huko, nasi twa—twawafurahia. Na—hapa kunao wengine tena wawili wanaokwenda kufanya—kuwa na ibada kwa ajili ya watu wa huko. Nasi—twafurahia mambo haya. Bwana awabariki sana.

¹⁹ Wengi sana, natazama na kuona watu mbali siwezi kuyataja majina yao wote, lakini najua kuwa Yeye awafahamu.

²⁰ Sasa naamini ikiwa dada yetu, mpiga kinanda, au mmoja wao atakuja hapa na kutupigia:

Kaa la moto lilipomgusa nabii,
Likamfanya kuwa msafi kama usafi uwezavyo
kuwa,
Na sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani
atakayekwenda kwa ajili yetu?”
Ndipo yeye akajibu, “Mimi hapa, nitume
mimi.”

²¹ Tunapowatawaza hawa wahudumu kwa kuwawekea mikono . . . Sasa, twatambua kuwa njia ya kimaandiko ya kumtawaza muhudumu ni kumuwekelea mikono. Nadhani kuwa hapo ndipo wale ndugu zetu wa Mvua ya Masika, au watu wa Bettelford na wengineo, walitatanishwa na—walipoona huko kuwekea mikono ili kugawia vipawa vya kiroho. Sasa, hatuamini kuwa vipawa huja kwa kuwekewa mikono. Twaamini kuwa kuwekewa mikono ni kibali kwa kile tumekwisha ona. Mwaona? Ni “amina!” Mwaona?

²² Basi, walipomwekea mikono Timotheo na juu ya hao ndugu, wao walikuwa wametambua ndani ya hao kulikuwamo kipawa. Kumbuka, “Chochea hiyo karama, iliyo ndani yako, iliyotokana na nyanya yako Loisi.” Nao walikiona hiki katika Timotheo, na kwa hivyo, wale wazee walimwekea mikono na kumtawaza, si kumwekea mikono mtu ambaye hamna kitu kilichoonekana wazi. Mwafahamu? Nao waliomba baraka, nasi sote twaamini hilo. Kwa hivyo hatugawi vipawa vya kiroho, tunavitambua

tu na kuwekea mikono yetu juu yao ili kukubali, ya kwamba twaamini kuwa Mungu ametenda jambo kama hili kwa watu.

²³ Nilitambua asubuhi hii huko mbali nyuma, Ndugu McKinney kutoka... (naamini ni Kinney au McKinney)—mhudumu Mmethodisti, anayeketi nyuma huko, hivi majuzi alitawazwa hapa pia (naamini kuwa hilo lilikuwa sahihi, kutoka jukwaani), ili kuwa huko Ohio na Ndugu Dauch na Dada Dauch, na lile kundi toka huko Ohio. Jamani, tukutanikapo pamoja hapa mahali padogo sote, tukija pamoja, ni ajabu. Bila dhehebu, hakuna kufungwa na kitu fulani, ila tu Yesu Kristo, huyo tu (mwaona?), kuketi tu pamoja katika ulimwengu wa roho.

²⁴ Vema, Dada, ukitupa... Hebu tu tuimbe hiki kifungu kimoja cha huo. *Kaa la moto lilipomgusa yule nabii*. Hebu tuuimbe pamoja sasa.

Kaa la moto lilipomgusa yule nabii,
Likimfanya awe msafi kama usafi uwezavyo
kuwa,
Sauti ya Mungu ilipouliza, “Ni nani
atakayekwenda kwa ajili yetu?”
Ndipo yeye akajibu, “Mimi hapa, nitume
mimi!”

Nena Bwana wangu! nena, Bwana wangu;
(sasa ndugu, mje mkiweza).
Nena, nami nitakujibu upesi...
[Makutano waendelea kuimba—Mh.]

²⁵ Na ndugu wengine wanaohudumu waje mbele, wakiweza, watakaowawekea mikono... washirika wa Maskani haya; Ndugu Ruddell, Ndugu Lamb, na wengineo.

Nena, nami nitajibu, “Bwana nitume mimi.”
Jamani mamilioni hivi sasa wafa katika
dhambi na aibu;
Sikiza vilio vyao vya uchungu na huzuni;
Hima, ndugu, upesi mwaokoe
Jibu upesi, “Bwana, mimi hapa!”
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu;
Nena, nami nitakujibu upesi.
Nena, Bwana wangu; nena, Bwana wangu;
Nena, nami nitajibu. “Bwana nitume mimi.”

Jina lako nani, ndugu? [Ndugu huyo asema, “Orlando Hunt.”—Mh.] Ndugu Orlando Hunt, kutoka Jiji la New York. Sivyo? Na Ndugu... [Huyo ndugu mwingine masema, “Joseph Coleman.”] Joseph Coleman.

²⁶ Sasa, mkiweza geukeni kuwatazama wasikilizaji, ndugu zangu. Ndugu Hunt na Ndugu Coleman, wito wa Mungu mioyoni mwao. Na kama tu vile tumeimba wimbo ule, “Kuna mamilioni sasa wafa katika dhambi na aibu,” wao wamesikia huo mlilo wa

huzuni na wa uchungu. Nasi twawauliza, “Hima Ndugu, upesi muwaokoe.” Mwaona? Jibu upesi, “Bwana, mimi hapa!” Hivyo ndivyo wao wanavyojibu asubuhi hii.

²⁷ Nasi kama ndugu wa kanisa hili, na kundi hili, twakubali hili kwa kuwawekea mikono yetu juu yao na kuwapa mkono wa kuume wa ushirika, kama—wawe washuhuda wa Yesu Kristo nasi tukiwaunga mkono hapa; kuwa tutawasaidia katika kila jambo lililo la heshima na jema katika Injili. Maombi yetu kila mara yatakuwa kwa ajili ya watu hawa kuwa Mungu atawatumia kwa kumheshimu Yeye. Na huduma yao iwe yenye baraka na kuu huko New York. Na maisha ya—yao yawe yaliyojawa huduma kwa ajili Yake, wakileta mavuno ya dhamani katika Ufalme. Na waishi maisha marefu na yenye furaha. Na Bwana Mungu awatunze kwa Uwepo Wake wa milele, na awape afya na nguvu na awaweke katika huduma Yake hadi Yesu Kristo atakapowaita kwa nyumba ya milele katika mbingu ya raha.

Na haya makutano sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu, nasi wahuduma twende mbele kuwawekea mikono... [Ndugu Branham aondoka karibu na maikrofoni awawekee mikono hao ndugu wawili—Mh.]

²⁸ Baba yetu uliye Mbinguni, twawekea mikono yetu juu ya Ndugu—katika Jina la Bwana Yesu Kristo, kwa kuwa yote tumejua kumhusu yeye Bwana yamekuwa ya haki. Nasi twakushukuru kwa wito huu wa huduma maishani mwake. Bwana, nena kupitia kwa ndugu huyu, walete watu, leta ukombozi, Bwana, kwao walio mateka wa magonjwa na—na kimawazo, na kimwili, na kiroho. Bwana, mpe huduma kweli kweli, ili aweze, mwishoni mwa njia yake, kutazama nyuma katika huo mkondo mrefu na aone kuwa yeye ameweza kwa neema ya Mungu kumteka kila adui. Twaomba katika Jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Amina!

²⁹ Juu ya Ndugu Coleman, twamwekea mikono pia kama mashahidi, Bwana, kuukubali wito wake, ambao sisi, kanisa hili, hili kundi la watu, twaamini kuwa yeye yu mtumishi wa Kristo. Nasi twaomba kuwa umbariki na umpe huduma kuu yenye nguvu, kuwa atawaleta watu kwa Bwana Wake, na kuwakomboa mateka, na kuvunja nguvu za Shetani zinazoyazunguka maisha ya watu anaoshirikiana nao. Bwana, mpe, maisha yenye matunda, afya zuri na nguvu. Na pia, afikapo mwishoni mwa njia, Mungu, ruhusu kuwa ataweza kutazama chini kwenye mkondo mrefu kuona ambapo neema ya Yesu Kristo imemwezesha kuvunja kila mnyororo wa adui kumheshimu Mungu.

³⁰ Baba wa Mbinguni, na hawa watu sasa waishi na kufanya kazi katika mavuno ya Mungu. Na baraka zako zikae juu yao na ziwe nao hadi wakati tutakapokusanyika miguuni pa Bwana wetu mkuu. Twaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina!

³¹ Mungu akubariki Ndugu Hunt, akupe huduma yenye matunda. Mungu kubariki, Ndungu, na akupe hu—huduma yenye matunda pia, Ndugu. Mungu awabariki. Tena

Kaa la moto lilipomgusa yule nabii,
Likimfanya awe msafi kama usafi uwezavyo
kuwa,
Sauti ya Mungu ilipouliza, “Ni nani
atakayekwenda kwa ajili yetu?”
Ndipo yeye akajibu, “Mimi hapa, nitume
mimi.”

Ee, nena, Bwana wangu; (Na Yeye anene na
moyo mingi michanga,) nena, Bwana wangu;
(Walioitwa na Mungu)
Nena, nami nitakujibu upesi.
Nena, Bwana wangu; nena Bwana wangu;
Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

³² Twamshukuru vipi Bwana asuhuhi hii kwa hii heshima kuu ya kanisa kushuhudia kutumwa kwa wahudumu uwanjani katika hizi siku za mwisho. Neema ya Mungu iende pamoja nanyi, ndugu zangu. Natumai Yeye atawatumeni katika nchi za kigeni na kote ulimwenguni, mkihubiri huu utajiri wake Yesu Kristo usiopimika, mahali unahitajika sana. Dunia leo ni hitaji sana.

³³ Sasa, kuna mengi ya haya mambo mazuri, itatubidi tu tuchukue machache hapa na machache pale, ili kuyaweka yote katika ibada asubuhi ya leo. Sasa leo tuna . . . ninanena kuhusu somo ambalo nime . . . Wakati mwingine sipendi kufikia huu wakati wa kuogofya sana.

³⁴ Basi, Jumapili iliyopita ikiwa wengine wenu hawakuwepo hapa na—na hawakupata ule ujumbe wa *Kule Kutoka kwa Tatu* [LILE NENO LILILONENWA Kitabu 2 Nambari 21—Mh.], na ikiwa mwapenda kanda, naamini mtafurahia hiyo moja; *Kule Kutoka Kwa Tatu*.

³⁵ Tuna nini hapa? Mvulana mgonjwa hapa, au kitu fulani? Ah, mvulana mdogo aliyelemaa. Naam! Mungu na ambariki. . . ? . . . Vema. Mwisho tu wa ibada tutawaombea wagonjwa, msijali. Mwaona? Kwa hivyo sisi . . . Sasa . . .

³⁶ Tuna—twawauliza, labda mkiweza, mpate ujumbe wa *Kule kutoka Kwa Tatu*, mara ya tatu ambapo ile Nuru, yule Malaika wa Bwana, ambaye amewaita watu kwa kutoka, amejionyesha mwenyewe dhahiri duniani katika kutoka fulani. Mwaona? Nadhani hilo ni jambo dhahiri sana kwangu: *Kule Kutoka Kwa Tatu*.

³⁷ Je, mngejali kama ningetoa koti langu? Ni joto sana humu katika Maskani haya asubuhi hii, na kurekebisha kwa hewa pekee tulio nako ni—ni kule ungejipepea. Yabidi utoe nguvu zako mwenyewe. Kwa hivyo tunapanga siku fulani kutengeneza

mpango kupafanya hapa ndani pawe baridi, upesi tuwezavyo kurekebisha mambo.

³⁸ Sasa, tungefurahiwa ikiwa mnge—mkipenda—kusikiza ujumbe huo, *Kutoka Kwa Tatu*. . . Sasa, tumekuwa na kutoka kwingi, lakini twaweza bila shaka kuweka mkono wetu mahali pale, wakati wa kutoka kutatu ambapo Mungu, katika hali ya Nguzo ya Moto, ameshuka kuwaita na kuwatenga watu. Na sasa. ni kutenganisha watu.

³⁹ Nasi twaona kuwa Yeye alipoita kutoka kule kwa kwanza, Yeye aliwatangulia katika Nguzo ya Moto na kuwaongoza hadi—kuwaongoza hadi kwa nchi fulani, halafu baadaye akawatokea katika umbo la Mwanadamu aliyeitwa Yesu Kristo. (Yeye alitoka kwa Mungu na alirudi kwa Mungu.) Na—ndipo alikataliwa. Naye alikuja wakati huo kuwaita watu toka kwa—toka katika desturi walizokuwa nazo, kama walivyokuwa huko Misri: wao walijitolea kwa dhambi na kwa—kwa njia za Wamisri. Na Mungu akawatoa.

⁴⁰ Na sasa, twapata mara ya pili walianguka katika utumwa kwa—Milki ya Kirumi. Ndipo wakaanza kuziendea kanuni za imani na wakaacha unyofu halisi wa ibada, na Mungu tena akaleta kutoka kwingine. Na—Yule—Yeye alionekana katika umbo la Mwanadamu aliyewaongoza wanadamu.

⁴¹ Katika kutoka kule kwa kwanza Yeye alikuwa Nguzo ya Moto. Ndipo Yeye alipokuja duniani katika yule Mwana-kondoo, hadi Yeye akawaongoza. . . Ni mfano mzuri vipi utakavyokuwa katika ule Utawala wa Miaka Elf, ambako Yeye analiongoza Kanisa sasa. Tutamwona Yeye kama alivyo. Tutakuwa na mwili kama mwili Wake wa utukufu.

⁴² Na leo kwa ile Nuru ya Injili ikirudishwa toka kwa Nuru fulani, Nguzo ya Moto ikionekana wazi kati yetu. . . Sayansi imeiona; iko katika magazeti na kote ulimwenguni; na imetambulikana kisayansi na kiroho kama Nguzo ya Moto ile ile, kwa ishara zile zile na mambo yale yale iliyoyafanya kila mara.

⁴³ Na sasa, katika siku ambazo kuna upotokaji wa akili mwingi na mengineyo, bali, Mungu kila mara hujitambulisha Mwenyewe. Sasa, twapata hili, na ni jambo la fahari vipi kujua kuwa haya maskani ya kidunia siku moja, huu mwili mdhaifu ulio mzee ambao sisi huwa wagonjwa na kuteseka ndani yake, utageuzwa na kufanywa uwe kama mwili Wake Mwenyewe wa utukufu. Ndipo tutamwona Yeye kama alivyo na kuwa pamoja Naye katika nchi tunayoiendea leo. Lo, ni. . . karibu latufanya tujisikie kama twaweza kusimama na kuimba, *Naelekea Nchi Ya Ahadi*. Labda wataimba huo huko katika ibada ya ubatizo hata hivyo, kwa sababu huo ni wimbo wetu wa ubatizo.

⁴⁴ Sasa kwa ndugu, walio hapa na katika nchi ambamo tepe hizi zitakwenda (na hiyo ni kuzunguka ulimwengu), jumbe hizi hazielekezewi mtu fulani. Na hatutaki watu wadhani kuwa sisi

tu aina fulani ya jamii au kundi la waliorukwa na akili ambao wamekuwa—tumekusanyika pamoja kujitenga, labda kwamba hatuna imani, au kujitenga wenyewe kumpinga mtu ye yote, au—wala kumpinga Mungu, wala kupinga kanisa. Sisi tu upande wa kanisa, lakini tunajaribu tu kuonyesha, kwa Roho Mtakatifu, na msaada Wake, sababu ya mtengano huu tulio nao sasa. Sisi—hatuuamini. Twaamini kuwa makanisa yote yabidi yawe yakishirikiana pamoja, sio kutengana, wamethodisti kwa kundi lao, Wabatisti kwa lao, na wa umoja, na wa utatu na *wengineo*, wote wametengana. Twaamini kuwa yapaswa yawe pamoja kama Mwili mmoja mkuu, wa kundi lililoungana la Yesu Kristo likingoja kuja huko kwenye utukufu. Hawapaswi kutengana hata kidogo.

⁴⁵ Na kile kiwatenganishacho, lazima kuwe na sababu moja ya kutokuwa pamoja. Na kwa kusoma, natambua kwa kusoma, si rangi ya ngozi zetu; kwa sababu wa manjano, weusi, wa hudhurungi, weupe, wote hutawanyika katika madhehebu mbali mbali. Si aina ya vyakula tunavyokula; sisi sote hula vyakula vile vile, twavaa aina ile ile ya mavazi, na kadhalika. Lakini naona ilipo—ilipo hasa, ni mtu aliyeiacha njia iliyowekwa ya mafundisho ya Injili. Kila mtu... Na yabidi kuwe njia fulani ya kuonyesha kabisa ni ipi iliyo kweli na iliyo makosa. Na jambo pekee utakalotenda, ni kutoweka tafsiri yo yote kwa Neno, lisome tu jinsi lilivyo, na uliamini hivyo. Kila mtu akiweka tafsiri yake mwenyewe hulifanya linene jambo lingine tofauti.

⁴⁶ Inalirudisha kwa dhehebu asili la kanisa Katoliki, ambapo kanisa Katoliki huamini kuwa Mungu yuko katika Kanisa Lake, na Neno halihusiki kwa vyo vyote vile, na Mungu yuko kanisani Mwake. Nasi Waprotestanti, kama tuonavyo katika Ufunuo 17 ya kwamba wao wote walikusanyika pamoja na ya kwamba kanisa Katoliki lilikuwa mama wa madhehebu yote. Nasi tuliona kuwa madhehebu ya Kiprotestanti, yangali yamepofuka, kipofu, yana hali ile ile ya kanisa Katoliki. Biblia yaita kanisa Katoliki kahaba na yaita kanisa la Kiprotestanti makahaba. Yasema kuwa yule kahaba alikuwa mama wa makahaba. Na hao ni, watu, yaani mwanamke wa sifa mbaya, asiyeishi akiwa mtiifu kwa ahadi zake za ndoa. Nasi sote twadai kuwa Bibi-arusi wa Kristo, na hali si waaminifu. Ni nini kingesababisha kutokuwa na uaminifu huo? Kwa kuishi kinyume cha—cha uadilifu ambao Mungu amemwekea Bibi-arusi Wake aishi kwake (hilo ni wazo langu), Biblia. Na ni Neno lisilokosea la Mungu, naamini. Na kwa hivyo, twaona kuwa kanisa la Kiprotestanti, ili liwe na dhehebu, lajitenga lenyewe hata na Maandiko ili kujifanyia dhehebu.

⁴⁷ Wahudumu, waliotawazwa, watashikilia mambo ambayo wao... Ah, wao huja chumbani mwangu cha kusomea, na vyumbani kwa mamia na kuniambia, “Ndugu Branham, wewe

huwahimiza watu. Hakuna yeyote anayeweza kuyapinga hayo huko. Wao wajua ni kweli.”

“Mbona,” nasema, “mbona—mbona hamfanyi hivyo?”

⁴⁸ “Vema, waona, nikifanya hivyo nitakuwa nikiomba mkate wangu. Hakuna ye yote... Nina huduma; yanipasa nimfikie Bwana. Na yanipasa niwafikie watu. Nami sitaungwa mkono.”

⁴⁹ Je, mwatambua tu kuwa Kristo ndiye muunga mkono wetu, Biblia ndiyo ituungayo mkono. Mwaona? Lakini ni... Basi lafanya kanisa la Kiprotestanti kitu kile kile hasa kanisa Katoliki lilicho.

⁵⁰ “Kanisa Katoliki halijali...” Vema, sisemi... Silifanyi kwa ujeuri hivyo, kusema hawajali yale Biblia husema. Wao—wanaamini Biblia, lakini (Mwaona?) wana... uhalifa wa kimitume ndio ulio msingi wa kanisa Katoliki; huo ni uhalifa wa “papa”, na kuita Petro “papa” wa kwanza na kuendelea. Naam, wao—huamini hilo, wao—wao huamini hilo kikamilifu.

⁵¹ Na Waprotestanti (mwaona?), wao—hukusanyika pamoja na kuwa na dhehebu kama tu walivyofanya huko Nikea, Rumi, ambako waliunda ka—kanisa Katoliki kwa—huko kwa Baraza la Nikea. Nasi twaona kuwa yote ni sawa; yote mawili ni sawa; wao huliacha Neno la Mungu watengeneze dhehebu. Mwaona? Na kisha ifikiapo Kweli nyingi kuu, ambazo zaonekana geni leo, ni geni kwao, kwa sababu wamefundishwa tu kwa kawaida za dini. Hatuna kawaida za dini ila Biblia. Hatuna cho—chote ila Neno Takatifu la Mungu, na hapo ndipo tunaposimama.

⁵² Naam, leo nataka kusoma baadhi ya Maandiko, kwa dakika moja hivi, toka kwa Neno takatifu, lililowekwa wakfu la Mungu, linalopatikana katika kitabu cha Injili ya Luka Mtakatifu, sura ya 23 ya Injili ya Luka Mtakatifu, kuweka msingi—kupata—kupata jukwaa ya yale nina—ninayotaka kusema, wazo la msingi kwa jambo ninalotaka kuongea juu yake. Na sasa mnafungua Luka Mtakatifu Sura ya 23. Nami nataka kusoma kifungu kimoja; hicho tu ndicho nahiutaji kwa msingi asubuhi hii kuweka hili juu yake. Sasa tunasoma sura ya 20—sura ya 23, na kifungu cha 33 cha sura ya 23.

Na wali... pofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulibisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume, na mmoja upande wa kushoto.

⁵³ Sasa, nataka kuyachukua maneno manne toka hapo, toka kwa hilo somo kuweka msingi kwa yale nataka kusema; hapo wao walimsulubisha yeye—maneno manne. Na somo langu linaitwa... Naleta shtaka kwa makanisa ya kidhehebu ya siku hizi na pia mengi ya yalio huru kwa kumsulubisha Yesu Kristo upya katika siku hii—kuwashtaki wao.

⁵⁴ Asubuhi hii linaitwa *Lile Shtaka*. Nami nataka nilitumie zaidi hivyo kama kwamba ilikuwa kama chumba, chumba cha

mahakama, ambapo kulikuwa na... Na hata hivyo, mimbara na kanisa ni chumba cha mahakama. Biblia ilisema ni kiti cha hukumu huko—huko... kuwa lazima ianzie katika nyumba ya Bwana. Na hii ni kama—kile kiti cha enzi na—na waamuzi na mashahidii, na wengineo.

⁵⁵ Nami ninalo leo, kama shahidi wangu lile Neno la Mungu, na shtaka langu ni dhidi ya makanisa ya siku hizi. Leo si—simleti mwenye dhambi katika hili; nazungumzia hili kanisa tu. Na itakuwa—kwe—kwenye kanda sasa, na—nitajaribu kufanya haraka niwezavyo.

Nakishtaki kizazi hiki kwa kumsulubisha Yesu Kristo mara ya pili!

⁵⁶ Na sasa, kutenda hili katika wakati huu tunaishi, ni—ninafanya... katika hili lazima nionyesha ushahidi. Ikiwa yanibidi nilete shtaka lazima uonyeshe ushahidi wa hatia ambayo imetendwa. Ni—nime... .

⁵⁷ Kuwashtaki ni—imebidi kuleta—ushahidi kulithibitisha, kuwa li—kuwa lile ninalosoma litasimama mbele ya yule Hakimku mkuu, ambapo... Nami najifanya mwenyewe kuwa wakili wa mashtaka kwa—kuhusu shtaka hili.

⁵⁸ Kuwa Neno la Mungu likiwa shahidi wangu, nakishtaki kizazi hiki kwa kule kumsulubisha. Lazima nionyeshe, na nitaonyesha, kuwa roho yule yule aliyetoa kusulubishwa kule kwa kwanza yuko juu ya watu leo na anatenda jambo lile lile. Na yanibidi kutenda hilo, ikiwa litakuwa sulubisho ambalo wamemsulubisha. Lazima niwaonyeshe ha—hawa watu kuwa hali ile ile iliyo katika watu leo inatenda jambo lile lile kiroho, walilolitenda kimwili wakati huo: walimsulubisha kimwili Yesu Kristo, yule Mwana wa Mungu.

⁵⁹ Na sasa, leo kwa Neno lile lile na kwa—kwa Roho Mtakatifu yule yule, na Neno lile lile, na natarajia kuyaonyesha makanisa wa—wao wanakosimama: kuwa wanatenda jambo lile lile leo; na Biblia ilisema wangelitenda; na kuthibitisha kuwa tunaishi katika siku hiyo.

⁶⁰ Haingetendeka miaka michache iliyopita. Nasema miaka hamsini iliyopita haingetendeka. Lakini leo hili liko kwa wakati wake hasa. Na halingalitendeka, labda, miaka kumi iliyopita, lakini laweza kutendwa leo, kwa sababu wa—wakati umekwisha. Tuko—tuko kwa wakati wa mwisho. Na naamini, kama mtumishi Wake, kuwa tuko—tumekaribia sana kuvuka toka nchi hii kuingia nyingine.

⁶¹ Kwa hivyo, wakati wa kutubu, kwa taifa, umekwisha naamini taifa hili haliwezi kutubu. Naamini kuwa limevuka mstari kati ya rehema na hukumu. Naamini linabatabata katika mizani.

⁶² “Ndugu Branham, kabla hujaanza kesi yako, utathibishaje hili?” Hivi tu: kuwa tuna hatia ya dhambi zile zile zilizomfanya Mungu akauangamize ule ulimwengu wa kabla ya gharika. Tuna hatia ya dhambi zile zile zilizosababisha Yeye kuuangamiza ule ulimwengu wa Sodoma na Gomora. Na sasa... Nasi tuna ushuhuda ule ule wa kiroho mbele yetu, ushuhuda ule ule wote wa kiroho, unaojulikana ulimwenguni kote, ulioshusha rehema za Mungu juu ya vizazi hivyo ambazo pia kuzikataa kulileta hukumu. Kwa hivyo ikiwa kizazi hiki kimekataa rehema ile ile iliyokataliwa katika siku hizo, Mungu hatakuwa mwenye haki akiwaacha waendeleo hivyo bila hukumu.

⁶³ Kama vile Jack Moore, rafiki yangu, alivyosema siku moja, “Taifa hili likiendelea tu pasipo hukumu toka kwa Mungu, basi Mungu hana budi kufufua Sodoma na Gomora na aombe msamaha kwa kuziteketeza.”

⁶⁴ Naam, twajua kuwa kiroho wanatenda jambo lile lile leo, maana wanalifanya kwa—kwa kusudi lile lile na kwa njia ile ile waliyotenda katika kumsulubisha Bwana, katika mwili. Wanatenda hivyo kwa ajili ya wivu, kwa sababu ya upofu wa kiroho, maana hawataki kuona; hawaisikizi. Yesu, katika safari Yake hapa duniani, Yeye alisema, “Isaya alinena vema kuwahusu ninyi; mna macho na hamwoni, na masikio na hamsikii.” Mwaona!

⁶⁵ Sababu ile ile, kusudi li—lile lile, mawazo yale yale, wanaleta kusulubishwa kwa Kristo upya tena (kama vile tutakavyoifikia muda si muda), kwa sababu zile zile walizolifanya wakati huo. Hawawezi kupata lo lote dhidi yalo; laiti wasingethubutu kubishana nalo. Nao wajua ushahidi uko hapo; nao wajua Biblia yasema hivyo; na jambo pekee wawezalo kufanya ni kulikufuru. Ndivyo hasa. Kwa hivyo... Na haya yote, sababu zile zile...

⁶⁶ Basi sasa, juu ya msingi huu nakihimiza kizazi hiki juu ya kusulubiwa kwa Yesu Kristo, kwa kumsulubisha, na wana hatia. Kwa mikono ya kidhehebu iliyo michafu, miovu, michoyo, wamsulubisha yule Mkuu wa Uzima aliyetaka kujijulisha Mwenyewe kwa watu. Mwaauliza, “Mtu yule yule?”

⁶⁷ “Hapo mwanzo kulikuwako Neno... naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili,” na kujidhihirisha Lenyewe. Lile Neno lilidhihirika katika mwili, nao waliuhukumu mwili na kuuua; kwa sababu lile Neno lilidhihirishwa. Waebrania 13.8 ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana leo na hata milele.” Ni Neno lile lile. Mwaona? Na kwa sababu ile ile wanajaribu kulisulubisha Neno.

⁶⁸ Naam, kwa kichwa changu cha maneno, kutenga-tenga maneno katika somo ninalotaka kulihubiri: *Hapo...* yale maneno manne. Hebu na tueleze *Hapo*. *Hapo*, ule mji mtakatifu sana duniani, Yerusalemu; *hapo* mji wa kidini sana duniani. *Hapo wao*, watu wa kidini sana duniani, katika karamu ya

kidini, ama ya Pasaka. *Hapo*, mahali pa kidini sana, mji wa kidini sana, dhe—dhehebu kuu la yote, kiongozi wa yote, hapo *wao*, watu wa kidini sana duniani, walikuwa wamekusanyika toka ulimwenguni kote. Wao *walimsulubisha*, kifo cha aibu sana kingalichoweza kuwepo—mtu angaliuliwa—uchi, walimvua nguo. Yeye—Yeye alidharau ile shutumu. Wao... Ule msalaba u—u—una kitambaa alichovikwa, lakini wao walimvua nguo Zake zote. Cha aibu sana... *Hapo* (mji mkuu sana wa kidini) *wao* (watu wa kidini sana) *walimsulubusha* (kifo cha aibu sana) *Yeye* (Mtu wa thamani sana).

⁶⁹ Ikiwa hilo halitoshi kukihukumu kizazi hiki! *Hapo*, dhehebu la kidini sana, lile kanisa kubwa sana kati ya makanisa yote lilikusanyika mahali pamoja; *wao*, watu wa kidini sana kati ya jamaa zote, watu waliopaswa kuwa waabudu halisi wa Mungu... Walikusanyika kwa karamu takatifu iliyo kuu zaidi waliyo nayo, kutakaswa kwa ile—ile Pasaka, walipotolewa kwa utumwa hadi kuwa huru. Na hapo katika wakati huo, *wao*, wakati huo watu wa kidini sana, na karamu ya kidini sana, katika mahali pa kidini sana, walimfanyia Mkuu wa Uzima jambo la aibu sana liwezalo kufanywa; kumvua mtu nguo zote na kumwangika mtini; kwa sababu, “Alaaniwe yeye yule... ilisema torati waliyoabudu kwayo, “Alaaniwe yeye yule aangikwaye mtini.” Naye alifanywa laana kwa ajili yetu. Wakamvua nguo Zake, wakimpiga, na kumdhihakiki, Mungu yule yule wa Mbinguni, wakimvua nguo Zake, na kumwangika msalabani... *Yeye*, hapo wao walimsulubisha Yeye chini ya adhabu ya kifo ya Kirumi.

⁷⁰ Kifo cha aibu sana leo hakingekuwa kupigwa risasi. Kifo cha aibu sana leo hakingekuwa—kugongwa na gari na kuuawa, kuzama majini, kuteketezwa kwa moto; lakini kifo cha aibu sana leo ni adhabu ya kuuawa hadharani, ambapo ulimwengu wote unakuhukumu na kukuita wewe mwenye hatia. Na ulimwengu mzima ulimtendea jeuri Mtu huyu na kumwita mwenye hatia hali Yeye hakuwa nayo. Naye alikufa kwa kusulubishwa na adui, sio na marafiki Zake, sio na sheria Zake, lakini sulubisho la adui, yule Mkuu wa Uzima, Mtu wa thamani sana aliyewahi kuishi, au atakayewahi kuishi. Yesu Kristo—*Yeye*, mtu wa thamani sana. Kumbuka hilo sasa tunapojenga jukwaa hilo leo.

⁷¹ Je waweza kuwaza, mahali kama Yerusalemu, ambapo kwa miaka 2,500 au zaidi, ambapo watu—au mamia ya miaka... Huenda nimetaja mingi zaidi. Huenda ilikuwa karibu miaka mia nane au mia tisa au kitu kama hicho. Sijui tu jinsi—muda gani tangu Suleimani alipojenga hekalu. Nakisia, yapata miaka mia nane, kitu kama hicho.

⁷² Nao walikuwa wakitazamia Masihi. Wao walikuwa wamekusanyika huko kwa ibada ya Pasaka. Hebu liwazie sasa: viongozi wa Mafarisayo wote, Masadukayo wote, na kadhalika, mkusanyiko mmoja mkuu kumwabudu Mungu. Mahali

patakatifu sana, Yerusalemu, hekalu la Bwana na watu wa Bwana wakamchukua Bwana Mwenyewe, na wakamsulubisha kwa adhabu ya kifo. Jambo gani hilo.

⁷³ Sasa, hayo maneno manne: wao—*Hapo wao walimsulubisha yeye*. Sasa ungali unaonyesha Biblia. Mwaona, ni maneno manne tu, lakini Biblia hubana Kweli Zake. Sasa mimi, yanibidi nizunguke hapa na pale na kueleza kile ninachonena, lakini Biblia haipaswi kufafanua chochote. Yote tu ni Kweli. Basi wao—ee—Biblia haipaswi kufafanua chochote. Haipaswi kufafanua, kwa sababu ni Kweli yote.

⁷⁴ Hapa kuna maneno manne ya mfululizo mkuu wa Kweli Yake. Nitajaribu kulieleza. Na kujaribu kulieleza dhahiri kungesababisha maktaba. Sina njia ya kuyaeleza haya maneno manne. Lakini sasa, hebu sisi, kwa msaada Wake Yeye aliyesababisha liandikwe, tujaribu kuyaeleza maneno haya manne, kuyaleta kwa njia fulani, ili watu walielewe.

⁷⁵ Tuna nini mbele yetu sasa? Tuna sulubisho la kwanza mbele yetu katika mahali patakatifu sana, watu wa kidini sana, kifo cha aibu sana, kwa Mtu wa thamani sana. Jamani, ni tatanisho jinsi gani! Lo, salala, ni fedheha!

⁷⁶ Sasa, hebu tuchukue neno la kwanza; *Hapo*. Hebu tulinene kwa dakika chache kabla hatujaleta shtaka. Tatalifafanua hili na kuwaonyesha kile walichokuwa wakitenda, ndipo tutakapotambua ikiwa shtaka langu ni sahihi au la. *Hapo*, Yerusalemu, patakatifu sana, mahali pa hekalu, kwa sababu hekalu ilikuwa huko; mahali patakatifu sana, kwa sababu—hekalu ilikuwa huko, na Wayahudi toka duniani kote alikusanyika mahali hapo pekee, mahali pa kukusanyikia kwa kuabudu. Mahali pakuu—pakuu sana pa kuabudia palipokuwepo, palikuwa Yerusalemu. Hekalu lilikuwa hapo. “Kama ilivyoandikwa imewapasa watu wote kuabudia Yerusalemu.” Vema, kwa sababu ni kituo kikuu cha kuabudia.

⁷⁷ Na leo mwasikia...Mmoja wao ataka kusema wao, “Lo, tunahudhuria mikutano hii mikubwa,” ambayo haya madhehebu yanayo. Na—na ndipo tuna kufunguliwa kwa—huko katika Mji wa Vatikani, na—na huku kutawazwa kwa “mapapa” na kadhalika. Wao, kila mtu asema, “Sisi sote twapaswa kwenda kwa vituo vya Wamethedisti au kwa—Biblia—mkutano Wabatisti,” au—au, “Yatupasa sote twende hu—huko Rumi.” Na huko ambako kuna kituo kikuu, wanavyokiita, cha Ukristo.

⁷⁸ Mnamo wakati wa vita vilivyokwisha, wakati Rumi ilianguka, hawa wanajeshi Wajerumani (wengi wenu vijana mwajua hili), hao wanajeshi Wajerumani walirudi katika Mji wa Vatikani hapo na kuwapiga risasi Waamerika waliokuwa wakiwakaribia. Ndugu Funk, na Ndugu Roberson, na wengi wenu, Ndugu Beeler, na wengi wa hawa ndugu

waliokuwa katika vita hivyo wanajua. Na mwajua nini? Tulitoa amri kuwa—wasipige risasi mji huo—Waamerika. Mlisimama hapo, nanyi mlikuwa shabaha yao; lakini huko West—kule Westminster Abbey, huko kwa—huko Uingereza, ungepiga risasi huko na haingejalisha. Hapo ndipo ambapo Waprotestanti walikusanyika, kwa hivyo ilikuwa vema kupiga risasi huko, lakini si kupiga risasi Vatikani; kwa sababu kama Rais Roosevelt... Nilisikia hotuba yake yeye alipo—yeye alipotangaza usiku huo, iliitwa, “Maongeo ya Mekoni.” Yeye alisema, “Rumi ilipoanguka,” yeye akasema, “aibu jinsi gani, kwa sababu Rumi ndiyo kichwa cha Ukristo wote.” Je, ungewaza Mprotestanti akisema hayo?

⁷⁹ Kwa hivyo kituo kikuu cha dini ya Kikristo... Vema, tuta—tuufanye huo kama Yerusalemu mkipenda. Mkipenda kufanya hilo, hebu tuufanye huo kuwa Yerusalemu. Kichwa cha haya mengine yote, lile—lile Baraza la Wazee na—na la Mafarisayo, na la Masadukayo, hao wote walikwenda huko Yerusalemu. Hayo ndiyo yalikuwa makao makuu hasa.

⁸⁰ Na katika maisha ya kidhehebu, yakubidi utambue kuwa Kanisa Katoliki la Kirumi ndilo mama yao wote. Hakika ni mama. Na lilianza toka Pentekoste, kwa sababu hapo ndipo walipofikia walipounda dhehebu. Sasa sisi, Waprotestanti tu dada wadogo waliotoka kwa kanisa hilo.

⁸¹ Na sasa, na tuseme ingekuwa hapa Vatikani leo, au huko Yerusalemu, kama ilivyokuwa siku hiyo, ambapo ilipasa watu wote waje Yerusalemu kua—kuabudu. Mbona walifanya hivyo katika siku za—za Yesu? Mbona wao walisema watu wote yawapasa waabudie Yerusalemu? Maana kuna mahali pamoja pekee ambapo Mungu atashiriki na wanadamu, hapo ni chini ya damu ya dhabihu. Hiyo ndiyo sababu iliwabidi waje Yerusalemu. Mungu hatakutana na mwanadamu pengine po pote, ila chini ya Damu. Ukataapo Damu, basi mahali pako pa kukutana na Mungu pameondolewa. Mungu alikata kauli Yake ya kwanza katika bustani ya Edeni, kuwa mwanadamu angemwabudu Yeye tu chini ya damu iliyomwagwa ya dhabihu. Hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu aliwahi kukutana na mwanadamu wakati huo, na ndipo mahali pekee Mungu aliwahi kukutana na mwanadamu; na hapo ndipo mahali pekee Yeye akutanapo na mwanadamu leo, ni chini ya Damu iliyomwagika ya Dhabihu. Mwaona?

⁸² Sijali ikiwa wewe u Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteria, ikiwa mwaweza kusahau tofauti zenu (Wakatoliki wa Kirumi, au chochote kile) na uje chini ya Damu iliyomwagika, Mungu atakutana pamoja nasi sote hapo. Hapo ndipo ambapo sote twaweza kukutana na kushirikiana katika msimamo ule ule. Lakini isipokuwa hivyo, Yeye hatakutana nawe tu kwa sababu wewe u Mmethodisti. Hatakutana nanyi kwa sababu mu Wapentekoste. Yeye atakutana nawe chini ya sharti moja; hilo ni

chini ya Damu iliyomwagwa, wakati dhambi zako zimekiriwa na kuondoshwa Uweponi Mwake. Ndipo kwa Damu. . . Na Damu kila mara iko mbele Zake, na kwa hivyo, Yeye aweza tu kukuona kupitia kwa hiyo Damu iliyomwagwa. Nawe u mweupe kama theluji (waona?) ukishakiri dhambi zako; la, sivyo, wewe huko hapo. Huwezi kushiriki.

⁸³ Hiyo ndiyo sababu huoni mambo yakitendeka makanisani; wanakiri kuwa wanaiamini Damu, lakini wanakataa mpango ule ule wa kupata ile Damu, Neno. Mwaona? Kunayo njia moja pekee ambayo Mungu ataheshimu Neno lile. Huwezi kamwe kuliheshimu lile Neno, ukija na kusema, “Mimi ni Mkatoliki wa Kirumi; nasisitiza *hili* litendwe.” Huwezi, Mmethodisti, Mbatisti, au Mpentekoste, huwezi kufanya hivyo. Njia pekee uwezayo kufanya ni chini ya huruma za Mungu kwa neema Zake, ni kwa Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo. Useme, “Bwana, naidai ile ahadi.” Waona? Na ndipo ikiwa u chini ya Damu hiyo hakika Mungu ana wajibu wa kutimiza Neno hilo. Lakini kwanza, yakubidi uwe chini ya Damu ile. Mwaliona sasa?

⁸⁴ Si ajabu hawawezi kuamini miujiza. Si ajabu hamwezi kuyaamini ya kimbinguni. Si ajabu wanailaumu. Sababu ile ile waliyoilaumu nyuma huko ndiyo sababu ile ile wanailaumu leo. Mna hatia kama hatia iwezavyo kuwa, kwa sababu chini ya Damu iliyomwagika tu. . . Nao wale wangethubutu. . . Maskini ndugu fulani, ambaye kwa unyenyekevu atii lile Neno la Mungu, na kwenda huko, na kuungama dhambi zake, na kusahau mafundisho haya yote ya sharti na kadhalika, na asimame hapo chini ya Damu, na kuliadini, ndipo wao wataka kumwita aliyerukwa na akili. Wao wanataka kumfananisha na kundi—ka—kama vile tugesema (si neno nzuri kulumtia mimbarani, lakini ni—na ili mfahamu), yeye ni wa kipekee. Na vivyo kuwa sisi tu wa kipekee. Mwaona? Muumini ni wa kipekee kwa asiyeamini, na asiyeamini ni wa kipekee kwa muumini. Kwa hivyo ni nani wa kipekee? Mwaona? Mkulima ni wa kipekee kwa mfanyi biashara; naye mfanyi biashara ni wa kipekee kwa mkulima. Mwaona? Kwa hivyo, yeye yu nani basi?

⁸⁵ Nawaambieni, wokovu ni jambo la kibinafsi kati ya mwanadamu na Mungu pekee: mtu binafsi, tukitafuta wokovu wetu kwa kuogopa na kutetemeka. Nami sijui msimamo mwingine, kama mwalimu asubuhi hii, au kama mhudumu toka kwa Kristo, ila kuuwekelea juu ya Neno. Siwezi kuuweka kwa jambo lingine liwalo lote.

⁸⁶ Sasa, twaona hapo, basi, kuwa chini ya damu pekee, ndipo Mungu amkutapo mwabuduo, kwa hivyo walikutanika Yerusalemu. Na Kristo ni Mwana-Kondoo wa dhabihu aliyetolewa na Mungu. Na leo, kuna mahali pamoja pekee ambapo Mungu atamkuta mwanadamu, na hapo ni chini ya Damu ya Yesu Kristo. Pengine po pote pamekataliwa; Mungu hatayasikia. Waweza kufanya kila aina ya—mwamsho, na kila

aina ya *vyama*, na kutetemeka, na kuruka, na uwe na damu na moto na moshi na kila kitu; lakini mradi tu maisha hayo hayalingani na lile Neno, naye Mungu akayadhihirisha maisha hayo kikamilifu; basi hakuna haja ya kuyajaribu haya, kwa sababu uko nje. Na Mungu hatakutana na hayo hadi yaje chini ya ulinzi wa Damu hiyo. Ndivyo.

⁸⁷ Kwa hivyo mwaona, katika Maandiko tuna Yerusalemu, (Kanisa linayo); ni Mbinguni, Yerusalemu ya kimbinguni, ambako Mungu yu Mungu. Na leo, si chini ya kanuni za imani wala chochote kile tunachojaribu kukifanya Yerusalemu. Tungependa... Wamethodisti wangependa kuto—wangependa kufanya makao makuu ya Kimethodisti Yerusalemu; Wakatoliki wangependa kufanya Rumi. Na—na mahali mbalimbali ambapo tuna makao yetu makuu, tungependa kupafanya hapo Yerusalemu yetu. Lakini Biblia yasema kuwa Yerusalemu yetu yatoka juu, ambayo ni mama wa waumini wote.

⁸⁸ Sasa, na Kristo ni Mwana-Kondoo aliyetolewa na Mungu. Oneni vile lilivyokuwa la kufaa sasa, kuonyesha kuwa hiyo Yerusalemu ilikuwa ikikoma. Lini? Ilikuwa ingali yafaa hadi saa hiyo; damu ya mwana-kondoo ilikuwa na maana hadi siku hiyo. Lakini sasa, katika kusulubishwa inabadilika. Taratibu za kale zimekwisha. Kulikuwa na mpya, na yu—yule Mwana-Kondoo alikuwa kwenye madhabahu. Yule Mwana-Kondoo, yule Mwana-Kondoo wa dhabihu alikuwa ardhini. Wao walikuwa wakimlaumu na wakitenda jambo lile lile hapo ambalo liliwabidi watende. Naam.

⁸⁹ Mungu abarikiwe kwa kuiona hii Nuru ya ajabu ya kimbinguni ya siku hizi za mwisho, kwa sababu makanisa yanatenda jambo lile lile leo. Hadi saa ambayo dini za kimadhehebu zimehukumwiwa na kuthibitishwa kuwa zinamtoa dhabihu Neno la Kristo, tokea hapo na kuendelea laja Neno na Neno pekee. Tangu... Yule mwana-kondoo wa kale wa pasaka akaondoka, na Kristo akawa Mwana-Kondoo wetu siku ile ya kusulubiwa. Na siku ile dhehebu liliposulubisha Neno la Mungu na likakubali kanuni ya imani badala ya Neno, hiyo ndiyo siku ile Neno lilitimilika kabisa. Hapo ni hivi majuzi tu.

⁹⁰ Tazama la pili: kwanza, *Hapo*, Yerusalemu; Pili, *wao*. Wao kina nani? Wayahudi, waabuduo. Waza hilo. Waabudu wenyewe walikuwa wakimuua yule yule wa—wao walidai wanamwabudu. Ungewaza jambo hilo, watu wa busara kama makuhani, waliofundishwa, waliokuwa na shahada za udaktari hadi wao—labda... Wao—wao walikuwa hawana budi kutoka kizazi fulani kabla wao—au—au kabila fulani kabla wao kuwa kuhani. Sharti wawe Walawi. Baba zao walikuwa makuhani; babu wa babu wa babu, wa babu, wa babu zao walikuwa makuhani. Nao iliwabidi waishi maisha yaliyowekwa wakf, hadi yodi moja dhidi yao wangepigwa mawe. Hakuna huruma iliyoruhusiwa. Watakatifu? Hakika, lakini utakatifu wa kujitengenezea tu. Walifanya hivyo

ili kuonyesha uso wao kwa ajili ya kanisa lao. Ndani yao Yesu alisema, “Ninyi mmejaa mifupa ya wafu.”

⁹¹ Vile ningaliweza kuleta papo hapo kwa mtu anayejua hilo kuwa Kweli, Neno hili kweli, na atapatana kulihusu kusudi aonyeshe uso mbele ya dhehebu fulani. Nina haki ya kuwashtaki (Naam) kulingana na Neno la Mungu.

⁹² Tazama, *wao*, waabuduo, watu waliotazamia ile ahadi, watu waliokuwa wameitazamia katika miaka na nyakati nyingi walidumu katika Seminari bila kazi yo yote ila kuligawanya Neno kulingana na mafundisho ya seminari, nao walikuwa wameukosa ukweli halisi wake. *Wao*, makuhani, huduma ya siku hiyo; *hapo*, katika makao yao makuu, *wao* ile huduma ya siku hiyo ilikuwa ikimuua Mungu yule yule, Mwana-Kondoo halisi. Yule yule waliyedai walikuwa wakimwabudu, wao walikuwa wakimuua.

⁹³ Na leo, nashtaki hili kundi la wahudumu waliotawazwa! Katika kanuni zao za imani na madhehebu wanamsulubisha kwa watu Mungu yule yule wanayedai kwamba wanampenda na kumtumikia. Nawashtaki hawa wahudumu katika Jina la Bwana Yesu, juu ya mafundisho yao, yanayodai kwamba siku za miujiza zimekwisha, na kwamba Ubatizo wa Maji katika Jina la Yesu Kristo hautoshelezi na si wa kweli. Juu ya maneno haya yote ambayo wao wamebadili na kanuni za imani zao, nawashtaki wao kuwa wana hatia, na Damu ya Yesu Kristo juu ya mikono yao, kwa kumsulubisha upya Bwana Yesu mara ya pili! Wao wanamsulubisha Kristo kwa umma, kuwanyang’anya kile kitu ambacho wao wanapaswa wawape wao, nao wamebadili kitu kingine mahali pake, kanuni za imani za kanisa kwa ajili ya sifa.

⁹⁴ *Hapo wao, wao*, wale wanaopaswa kujua vema zaidi. Ikiwa mtu yeyote angepaswa kujua vema zaidi, ingekuwa wahudumu. Ikiwa mtu yeyote angejua vema zaidi, ingekuwa wahubiri wa siku hizi! Ikiwa mtu yeyote apaswa kujua, ma—maaskofu, na maaskofu wakuu, na—na wahudumu, na wenye shahada za elimu juu ya Mungu wapaswa wajue tofauti. Lakini mbona wao hawajui? Lo, ni jambo la kutatanisha vipi! Tuna nini mbele yetu hapa ila—ta—tatanisho? Wao wanadai kuwa wanamwabudu Mungu, nao wanamuua yule Mkuu wa Uzima.

Wao... *Hapo wao walimsulubisha Yeye*, na hapa *wao* tena wanatenda jambo lile lile, maana Yeye yu Neno. Hivyo ndiyo... Yeye ndiye kurudisha tu kwa lile Neno. Na hivyo ndivyo Yeye alivyo leo, kurudishwa kwa lile Neno, akijaribu kupata mtu fulani ili ajione Yeye Mwenyewe kama kwa kioo.

⁹⁵ Na watu hawa huwaweka makutano mbali na Mungu. Na—na kukiwako jambo lolote linalotendeka, na limenenwa katika yale makutano, wao hulilaumu toka jukwaani, toka mimbarani, na kusema, “Ni kurukwa na akili. Ondokeni kwalo.” Katika—

hivyo, wao walimsulubisha Yesu Kristo katika mwaka wa 1963, nao wana hatia tu kama watu wale—wa siku hiyo. Hayo ni maneno ya kuogofya, ila ni kweli.

⁹⁶ Kwa...Hivyo ndivyo vile hasa wanavyotenda leo. Na kwa sababu hii, kwa sababu ya kumsulubisha Kristo, kwa sababu ya kuchukua lile Neno, na kuliondosha kwa watu, ndivyo hasa walivyokuwa wakifanya pale. Neno lile lile ambalo Mungu alikuwa akilirudisha kupitia kwa Mwanawe Mwenyewe kuthibitisha lilikuwa ndilo, na ambalo wanadai kwamba walipenda, yule Yehova aliyejidhihirisha Mwenyewe kwa Maandiko, ametenda hasa yale Yeye alisema angetenda, yale hasa ambayo Mungu alisema angetenda, na kuyaonyesha mbele zao. Kwa sababu ya kupenda makundi ya kanisa lao na mambo kama haya, wao walimhukumu Mkuu wa Uzima. Nami nalihukumu kundi lile lile leo na kulishtaki kama wenye hatia mbele za—za Mungu, kwa lile Neno la Mungu kuwa wanatenda jambo lile lile. Kizazi hiki kimeshtakiwa.

Kumbuka Waebrania 13:8. Ni Yeye yule jana, leo na hata milele.

⁹⁷ Walimshtakije? Kwa sababu kanuni zao za imani hazingalimkubali. Na ndani mioyoni mwao walijua tofauti. Je, si Nikodemo, katika sura ya 3 ya Injili ya Yohana, alieleza vema? “Rabi, sisi, Mafarisayo, wahubiri, waalimu, twajua ya kuwa Wewe u mwalimu, kutoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya ishara hizi uzifanyazo Wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.” Mwaona? Wao waliishuhudia hadharani kupitia kwa mmoja kati ya watu wao mashuhuri. Ingawaje, kwa ajili ya kanuni za imani zao wao walimsulubisha Kristo. Na leo hakuna msomaji ambaye hawezi kusoma Matendo 2:38 kama vile mimi niwezavyo kuisoma, na mengineyo jinsi mimi niwezavyo kuyasoma. Lakini kwa ajili ya kanuni za imani zao na kwa ajili ya—ya tikiti zao za kidhehebu walizo nazo mifukoni mwao (ile chapa ya mnyama wanayoibeba kama kadi ya ushirika)...Na kwa kuchukua mambo hayo, wao humsulubisha Yesu Kristo upya kwao wenyewe, na kumsulubisha kwa umma; na kukufuru Mungu yule yule aliyeahidi kutenda hili, wakileta laana juu ya kizazi hiki.

⁹⁸ Hapo...Hapo *wao*, sio wenye dhambi, *wao*, hao ni, kanisa la siku hiyo, walimwonea makosa yule Mtu aliyekuwa ndiye lile Neno. Sivyo? Walimwonea makosa yule Mtu aliyekuwa lile Neno. Sasa wao hulionea makosa lile Neno likitenda kazi kupitia kwa mtu (oneni, wao wanatenda vivyo hivyo), ambaye alikuwa—katika mtu, huyu—Roho Mtakatifu anafanya kazi kumpitia, ni thibitisho la Mungu. Wao walijua kuwa Yeye ni Kristo? Kwa sababu kazi zake zilithibitisha alichokuwa. Yeye alisema, “Ni nani kati yenu awezaye kunishtaki kwa dhambi? Kama sijafanya hasa yale Maandiko yalisema ningefanya...Na ambayo...Mtu

fulani aniambie mahali fulani nilipoangukia, ikiwa sijaonyesha kila ishara ambayo—kuwa Mimi ndiye Masihi, kuwa Mimi ndiye yule hasa mliyahidiwa!”

Kasema, wao walisema, “Vema, tuna Musa. Twaamini Musa.”

⁹⁹ Kasema, “Mngalimwamini Musa, Mngeliniamini na Mimi. Ikiwa ninyi. . . Musa aliona siku yangu na—na akatamani ku—kuishi katika siku hii. Musa aliona mbali sana katika manabii. Na hapa mwaishi katika hiyo nanyi mnahukumu.” Kasema, “Ninyi manafiki,” kasema, “mwaweza kutambua uso wa anga, bali hamwezi kutambua ishara ya wakati.” Iko hapo, ishara ya wakati.

¹⁰⁰ Walimhesabia katika kundi gani? Aliyerukwa na akili, mwenda wazimu. Naam, walimwonea makosa Mtu Yule aliyekuwa ndiye Neno. Yeye alikuwa ndiye Neno. Injili ya Yohana sura ya kwanza yalithibitisha:

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu. . .

Naye Neno alifanyika mwili, na akakaa kwetu, . . .

¹⁰¹ Yeye alikuwa Neno lililo hai la Mungu, kwa sababu Yeye alikuwa akimdhahirisha Mungu kupitia Kwake Mwenyewe. Yeye alijisalimisha—kabisa—kwa Neno la Mungu, hata Yeye na Neno wakawa sawa. Na hivyo hasa ndivyo kanisa lipaswavyo kuwa leo, kuwa Neno la Mungu ni sawa. Waweza kuwa sehemu ya Neno hali unalikana lote kwa matendo? Na sababu lifanywavyo hivyo si kwa sababu ya watu. Hiyo ndiyo sababu nadhani Mungu alinena nami kuhusu kuita watu hawa “Wahuni” na “hawara.” Ni kwa sababu haya madhehebu choyo yamewafanya watu hao waishi hivyo. Wao waliisulubisha Kweli, na watu wanaiita kufuru—samahani, na wanaikufuru. Wanaiita kurukwa na akili na mengineyo, wasijue kuwa wanamkufuru Mungu yule yule wanayekwenda kanisani kumtumikia.

¹⁰² Hivyo basi, nashtaki kikundi hiki cha wahubiri leo. Nakishtaki kizazi hiki katika Jina la Yesu Kristo, chini ya mamlaka ya Neno la Mungu; mnamsulubisha tena.

¹⁰³ Tazama, ni Yeye yule jana, leo na hata milele. Neno la Mungu likithibitishwa katika mwanadamu.

¹⁰⁴ Linganisha Kalvari zile mbili na shtaka lao. Kumbuka, “Kwa sababu yeye alijifanya mwenyewe Mungu, hatumtaki mtu huyu atutawale.” Ni shtaka gani walilipata katika baraza asubuhi hiyo, walipomsulubisha Yesu? Kwamba Yeye alijifanya Mwenyewe Mungu—Yeye alikuwa Mungu; Naye alivunja Sabato—Naye alikuwa Bwana wa Sabato. Walimhukumu kwa sababu Yeye alijifanya Mwenyewe Mungu. “Huna haki ya kufanya hili. Huna haki. Makuhani. . . Ikiwa kuna chochote kinachokuja, kitakuja kupitia kwa makuhani wetu.

¹⁰⁵ Sasa, linganisha hilo na Kalvari leo. Wakati Mungu (ilimpendeza Baba, Mungu, yule Roho, kumwinua Mwanawe) alimfunika kwa kivuli yule—Mariamu kwa Roho Mtakatifu na akazaa mwili ambao ungemtumikia na kutimiza kusudi Lake ku... Yeye—Yeye... Yule Mungu alikuwa katika Kristo, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, katika Yeye akionyesha kile Mungu alichokuwa kwa watu, akiruhusu ule—akiruhusu ulimwengu wote ajue vile Mungu alitaka kila mtu binafsi awe: mwana na binti. Alimchukua Mtu mmoja na kutenda hili. Na kwa sababu Yeye hakujiunga na makundi yao ya kidhehebu, wao walimhukumu na kumsulubisha.

¹⁰⁶ Sasa linganisha hiyo Kalvari na leo! Kwa ajili ya kuonea kwa kidhehebu, kwa ajili ya tofauti kati ya wanavyuoni ambao wapaswa kujua lile Neno na mpango wa Mungu; kwa ajili ya haya, Mungu aweza kuchukua kundi la watu ambao Yeye aweza kuwatumia mahali fulani na kujijulisha Mwenyewe, watakaojinyenyekeza kwa Neno. Na wao hawawezi kusema sivyo ilivyo. Hawangeweza kusema Yeye hakulitenda, maana makutano yao ni mashahidi wa hilo. Lilikuwa mbele yao. Hawangeweza kulikana. Hawangekana madai Yake, kwa sababu Neno lile lile walilosema wanaliamini ndilo lile lililothibitisha alivyo Yeye, kwa sababu Mungu alilichukua lile Neno lililokusudiwa kuwa Masihi na kulionyesha kupitia kwa Mwanadamu. Nao iliwabidi wamwangamize. Njia pekee ambayo wangeiendea ilikuwa kumwangamiza yule Masihi. Nao walilitenda katika upofu na kutojua ingawa walikuwa na elimu yao. Wao walikuwa werevu, wenye busara, tukinena kilimwengu, kama tulivyowalinganisha usiku uliopita. Nuru ilipomgusa yule kijana tajiri, tazama kile alichotenda. Yeye aliiakataa—mtu mwerevu. Paulo, mtu mwingine mwerevu, Nuru ilimgusa. Je, yeye alifanyaje? Aliikubali. Yeye aliyasahau yote yale aliyoyajua, ili aweze kumjua Kristo. Hilo liliyafanya maisha yake yawe yastahiliyo Injili. (Ujumbe wa Jumapili iliyopita.)

¹⁰⁷ Vivyo hivyo leo. Yamgusa, labda, mwanamume fulani aliyekosea, alikuwa na wito wa Mungu, alivyojisikia, akaenda kwa seminari fulani na kujifunza kanuni fulani za imani. Yeye lazima azitii hizo kanuni za imani au arudishe kadi yake ya ushirika. Akifanya hivyo, yeye ana waa. Hakuna ye yote atakayemkubali, kwa sababu wakati mmoja alikuwa wa kitu fulani kingine: na sasa, hayuko huko tena. Wadhania mtu huyo ana kasoro fulani, na hawatamkaribisha katika makutano yao, wakati makutano yanatazamia ishara moja tu pekee, yaani: ikiwa yeye aamini yale waaminiyo. Ikiwa yeye ana kadi, ikiwa yu Mmethodisti... Ikiwa ana kadi—yeye yu wa ushirika mwingine, iwe umoja au utatu, au wowote ule, Church of God, au katika mashirika ya Kipentekoste na shirika hizo zote... Kama yeye yuna kadi, wao hujua kuwa makao yake makuu yamemchunguza, na kuchunguza akili zake, na kumfanyia

uchunguzi wa daktari wa akili, na kuona ikiwa kipimo chake cha busara ni kikubwa kutosha kunena mbele yao. Ikiwa yeye hayuko hivyo, wanamkataa. Naam.

¹⁰⁸ Lakini mwaona, makutano yapaswa yawe yakiutazama mkono wa Bwana: waone ikiwa Mungu amemtawaza au la. Hilo ndilo litupasalo kuchunguza. Lakini leo wao wanamsulubisha yu—yu—yule Mwana wa Mungu upya, wakati mtu wa Mungu yuaaweza kwa neema ya Mungu kuitwa na Mungu ku—kumwacha Mungu arudishe mng’ao Wake kupitia kwake. . .” Kazi nizifanyazo Mimi mtazifanya nanyi,” Yeye alisema.

¹⁰⁹ Tazama ni siku jinsi gani tunayoishi. Wao walichukua—wao walichukua ile—Kalvari ile ile (twaweza asubuhi hii) na kwa sababu ile ile. . . Sasa, walijua hilo lilikuwa ni Kweli, lakini kwa ajili ya wivu, kuonea. . . Yesu aliwaambiaje, “Ikiwa natoa pepo kwa kindole cha Mungu, basi nani—ninyi mnazitoa kwa nani? Hebu wao wawe ndio hakimu wenu. (Mwaona?) Hivyo nami ikiwa hutoa pepo kwa kindole cha Mungu. . .”

¹¹⁰ Sasa, kama tu ulivyosikia wao wakisema, “Je, waweza kuthibitisha ni kindole cha Mungu?” Ningalipenda, ningalipenda kusikia akiulizwa swali hilo. Wao walikuwa wajanja sana hawangalimuuliza hilo.

¹¹¹ Tazama! Kwa sababu Yeye alijifanya Mwenyewe Mungu (Naye alikuwa Mungu). . . “Nasi hatumkubali atutawale.” Lakini sasa jambo—mlio ule ule wa kale warudi tena. “Hiyo Biblia iliandikwa na wanadamu,” wao husema. “Haitubidi tuitii.” Hiyo ni ya Mungu—Hiyo ni Neno la Mungu; Ni Mungu Mwenyewe.

¹¹² Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani jana, kasema, “Vema, yawezekana mtu fulani aliandika Biblia hiyo.”

¹¹³ Nilisema, “Naam, aliiandika. Jina Lake. . . Twamjua Yeye kama Mungu.” Iliandikwa mbali mbali kwa muda wa, karibu miaka elfu nne, yale Maandiko, nyuma huko toka kwa Ayubu, hadi kwa Agano Jipya, na yaliandikwa kwa mamia kwa—kwa—na mamia ya miaka mbalimbali, na yaliandikwa na watu mbalimbali. Na wao bila kujuana, katika sehemu mbalimbali za nchi, na hakuna hata neno moja linalolaumu lingine. Nataka mtu yeyote aje chini ya ile Damu ya Yesu Kristo na adai ahadi yoyote ndani Humo. Mungu ana wajibu wa kuitunza. Lakini wao hawatafanya hivyo. Wao watakuja na kusema, “Ee, Bwana, nataka kufanya kitu fulani. Nipe kipawa kikuu. Haleluya, Bwana. Utukufu kwa Mungu! Naamini nimekipata. Haleluya!” Haitatendeka. Waweza kuleta elimu ya kusomea mawazo, lakini haitatendeka. Yapasa Mungu atambue kutubu huko; yapasa Mungu afanye hivyo. Tungesema mambo mengi yanayohusu hayo, lakini natumai mna. . . mnaifahamu.

¹¹⁴ Tazama! Bali sasa hawataki Neno liwatawale. Nasema, “Kila mmoja wenu arudi; mmebatizwa vibaya. Mmebatiswa katika kanisa Katoliki.”

¹¹⁵ “Wewe u nani hata utwambie hayo?” Si mimi; ni lile Neno. “Lakini nakwambia, sisi—twaamini. . .” Sijali mnaamini nini, ni yale tu Biblia isemayo, “Vema, haitubidi tuyatii hayo.” Myatii, la sivyo, mko chini ya hukumu ya Biblia hii, maana, “Yeyote atakayeliondoa neno moja toka Humo wala kuongeza neno moja Humo, yeye ataondoshwa, ile sehemu, ya Kitabu kile cha Uzima,” awe mhudumu, mhubiri, au ye yote yule. Yakubidi uje chini ya utawala wa hili Neno, maana ni Mungu. Biblia yasema ni Mungu. “Hatutaki litutawale.” Wao huchukua kanuni za imani zao na madhehebu, na mambo ya—yao madogo wanayoaamini na yamewekwa na baraza za wanadamu, na wanayachukua badala ya lile Neno la Mungu.

¹¹⁶ Je, walifanyaje? Wao walimchukua Baraba fulani, muuaji, badala ya Mwana wa Mungu, siku ile ya kusulubishwa kwa kwanza. Na leo wanalichukua neno la watu fulani, ambalo ni uongo na njia ya mauti, na wanakataa kuchukua njia ya Uzima, Neno la Mungu. Nakihukumu kizazi hiki, nakishtaki katika lile Neno la Bwana, kuwa wamekosea. Wana hatia ya kumsulubisha, au kujaribu kumsulubisha yule Roho. . .

¹¹⁷ Wao wanaita mkutano wa ufufuo kila mahali. Je, utakuwaje, na mkutano wa ufufuo hali Neno lenyewe haliwezi kufanya kazi, katika watu? Ningependa mtu fulani anijibu hilo. Yawezekanaje hali unakana ufufuo ule ule wenyewe? Nabii alinena vema juu yao, “mifano ya utauwa.” Taratibu zao wenyewe nyuma huko zilikana lile Neno la Uzima. Taratibu zao leo zakana kitu kile kile kiwezacho kuleta ufufuo, kanuni za imani na mifano. Naam, bwana! Wao huchukua dhehebu na kanuni zao za imani badala ya li—lile Neno, na hizo husulubisha Neno Lake na kulifanya Neno Lake lisiwe na nguvu kwa watu. Waonapo Neno la Mungu waziwazi katika (lajidhihirisha Lenyewe, kuwa Mungu alitoa ahadi ya kuwa angelitenda hili, na hapa Yeye analitenda)—nao wanalifanyia mzaha na kuliacha, ni kukufuru. Wao wanajaribu kusukubisha lile Neno Lenyewe. Kwa nini wanalisulubisha? Hawawezi kusulubisha Neno zaidi ya wasivyoweza kumsulubisha Mungu. Wangeweza kuusulubisha mwili alimokuwa Mungu, Mwana wa Mungu; wangesulubisha huo, bali hawawezi kumsulubisha Mungu. Yeye alifanywa hivyo wakati huo, kusudi awe dhabihu awaleta wana wengi waliochaguliwa tangu asili kwa Uzima wa Milele. Iliwabidi wamsulubishe wakati huo, lakini hawawezi kufanya hivyo sasa. Hawawezi kufanya hivyo, maana Neno Lenyewe litadumu. Bali wao. . .

¹¹⁸ “Wao wanafanyaje? Wao wanaundaje? Wewe, mhubiri wasemaje basi? Unajengaje msimamo wako hapa kuwa wao walimsulubisha wakati huo?” Wao wanasulubisha nguvu za

Injili juu ya watu kwa kanuni zoa za imani. Hilo ndilo sulubisho; ambako umati umewekwa katika hivi vyumba vikubwa vya maiti vinavyoitwa makanisa, madhehebu, na kutengeneza mipaka ya kanuni za imani, na hilo lilikuwa na—Neno la Mungu haliwezi kuwa na nguvu juu yao kwa sababu wao—wao wanayahukumu mambo yale yale Kristo aliyosema yangetendeka. Haiji kulingana na kanuni zao za imani na wala Yesu hakuja kulingana na kufahamu kwao juu ya kuja Kwake. Yeye alikuja kwa njia ile Mungu alimtuma, na alikuja hasa kulingana na lile Neno. Si ajabu Yeye alisema alificha mambo haya kwa wenye hekima na akili, akawafunulia watoto wachanga ambao wangejifunza. Je, mwafahamu? Lo, wao wamezisulubisha nguvu za lile Neno.

¹¹⁹ Nina mafungo ya Maandiko hapa. Huenda nikataja tu mawili au matatu yake. Wao walimsulubisha... Mwasema, “Walilisulubishaje Neno?” Yesu asemapo kuwa ni Yeye yule jana leo na hata milele, Waebrania 13:8, wao husema, “Kwa njia fulani Yeye yuko hivyo.” Mwaona. Vema. Na ikiwa Yesu alisema kuwa agizo Lake la mwisho kwa Kanisa ni: “Enendeni ulimwenguni mwote (Marko 16)—enendeni ulimwenguni mwote mkaihuriri Injili, ishara hizi zitawafuata hao waaminio,”... Ulimwenguni mwote kwa kila kiumbe, na haijaufikia nusu bado. Na kuna mamilioni wanaokufa kila mwaka ambao hata hawajawahi kusikia Jina la Yesu. Kwa hivyo lingali agizo kwa wote; lingali agizo la Mungu. “...Ulimwenguni mwote mkaihuhiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoka pepo; watasema kwa lugha mpya; watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Nao husema haya yalikuwa ya kizazi hicho, nao watangua agizo la Mungu kuhusu hili. Nao wasulubisha nguvu za Neno kwa watu. Amina!

¹²⁰ Petro alisema siku ya Pentekoste (akiwa na funguo za Ufalme ambazo Yesu alikuwa amempa, “Chochote usemacho hapa, nitakisema juu huko.”)... Na katika siku ya Pentekoste wao waliuliza watende nini ili wapate Roho Mtakatifu, kwa kuwa walikuwa wakiifurahia, wakishuhudia wengine wakitenda kile wangeita upuzi: wakiyumbayumba, wakirukaruka, wakianguka, wakitenda kama walevi. Nao husema, “Na watu wale wamelewa kwa mvinyo mpya.”

¹²¹ Lakini kulikuwa na mtu aliyesimama anayeitwa Petro, aliyekuwa na funguo za Ufalme, yeye alisema, “Sivyo mnavyodhani; (Matendo 2) watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililonenwa.” Mwaona? Arudi tena kwa Neno, akionyesha kuwa Roho yuangali Neno, na Neno lingali ni Roho, Neno la Mungu. “Itakuwa kama ulivyonenwa (kwa kinywa cha nabii Yoeli, Yoeli 2:28),

itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu.” Msikizeni huyo nabii akisimama pale. Mtazame, kwa ujasiri, akisimama hapo kwa kundi hilo na kulihukumu, kulishtaki. Kasema, “Hili ndilo lile lililonenwa na nabii, ‘Nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana wenu na binti wenu watatabiri; Nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho Yangu. Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu na katika dunia moto na minara ya moshi, na mvuke wa moshi.’” Kulithibitisha kwa Neno kuwa lilikuwa Neno, nao walicheka na kulifanyia mzaha, nao waliingia hukumuni; na mji huo ukateketezwa, nao wakawala watoto wao kwa wao. Na leo wao ni watu waliotowanyika ulimwenguni kote, kuonyesha kuwa Roho Mtakatifu bado yu Neno la Mungu kulileta Neno hili lipate kuishi.

¹²² Yesu Kristo alikuwa Mtu, Mwanadamu, Mungu. Haleluya! Yeye alikuwa dhahirisho la Mungu, Yeye alikuwa Mungu katika mwili ajirudishie lile Neno la Mungu kwa wakati huo, kufanya kizazi hicho kione ile ahadi ya Mungu kwa wakati huo. Na Roho Mtakatifu ndivyo alivyo leo; Ni Roho wa Mungu juu ya lile Neno lililoandikwa, akijaribu kumpata mtu fulani ajidhihirishe mwenyewe kwa wakati huo kuthibitisha kuwa ni Yeye yule jana leo na hata milele; Injili ya Yohana 14:12; “Kazi nizifanyazo mimi, ninyi nanyi mtazifanya”—Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo na hata milele. Mwaona? Kila mara linajaribu kutafuta njia yake kujirudisha Lenyewe.

¹²³ Na hawangelifanya. Watu wawaza sana kuhusu madhehebu yao, viota vyao vidogo walivyokuwa navyo na kadhalika, viitwavyo makanisa yao, kwa hivyo wao hawangemsikiza. Ndivyo wao wafanyavyo leo, jambo lile lile, kumsulubisha upya.

¹²⁴ Petro, katika siku ya Pentekoste alisema, “Ninyi nyote mkaao Yerusalemu, katika Uyahudi, mkasikize maneno yangu. Watu hawa hawakulewa. Mkitulia, nitawaonyesha ni nini.” Naye aliendelea na kwaeleza. Mioyo yao ilichomwa, waliposikia hili, walisema, “Tutendeje, ili tuokoke? Tufanyeje tupokee Hili? Tumeshawishika kuwa neno Lako Kweli.”

¹²⁵ Yeye akawaambia “Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hili ndilo lililowabidi watende: watubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

¹²⁶ Na leo, Kanisa Katoliki la Kirumi walishikilia, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” kuchukua mahali pake. Badala yake, ushirika—kutoa nje ulimi na kula ule mkate mwembamba wa duara, na yule kasisi anywa divai, nanyi mu mmoja pamoja. Ushirika, badala ya kuwa Roho Mtakatifu wanauita “Misa

Takatifu.” Na—“Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” ni ubatizo wa utatu, hali hata haujanenwa katika Biblia. Jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni Bwana Yesu Kristo. Na ukionyesha hilo kwa hiki kizazi chenye ukaidi, kama Petro alivyosema, “Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi,” ukiwaonyesha, wao wanafanyaje? Wanalifanyia mzaha na kusema, “Kanisa letu halifundishi hivyo.” Basi mna hatia, mna hatia ya kumsulubisha Yesu Kristo kwa kuziondolea mbali Nguvu za Mungu kwa watu. Mwasulubisha Neno lile lile kwao, nanyi mwajihukumu wenyewe na makutano yenu. Ni kuwaongoza mkiwaelekeza katika mtego wa mauti.

¹²⁷ Kama nilivyosema kuhusu huyo mhudumu Jumapili iliyopita, huyo alikuwa Martin Luther King huko na hao watu wapendwa, akiwaongoza waingie katika mtego wa mauti. Jamani, laiti mtu fulani angaliongea na mtu huyo! Laiti ningaliweza. Kwa ajili ya—ya ghasia ndogo kuhusu azimio la shule. Mwaona? Ni tofauti sana. Salala, watu wasipokuwa na moyo kutosha kushirikiana na mtu kwa ajili ya rangi yake, wamehukumiwa na wamekufa hata hivyo. Taifa linawapa haki... Usiipingie. Usiipingie...

¹²⁸ Vipi kama mtu fulani angesema Wa-Irish wote, au mtu fulani, Wajerumani wote, au mtu fulani apaswa kujitenga. Hilo halingewasumbua Wakristo; wangeendelea tu. Na mtu huyo ni Mkristo. Kama—kama mhudumu, haimbidi awaongoze watu wafanye ghasia kupinga hayo. Watasababisha vifo vya mamilioni. Itaanzisha uasi mwingine. Ni aibu kufanya hivyo.

¹²⁹ Jambo lile lile latendeka papa hapa. Jambo lile lile hasa tena. Hiyo ni kweli. Mwaona? Watu, laiti wangelitazama kweli pekee na kuona Kweli ni nini... “Kanisa letu haliadini hilo. Tuna njia nyingine.” Vema, si njia sahihi. Hiyo siyo. Hicho sicho kitu.

¹³⁰ Yeye alisema, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi.” Sasa, hawatalitenda. Lo, basi wao walifanyaje? Naam, hilo ni jambo moja tu kati ya mamia tutakayoyafikia, labda, upesi tuwezavyo.

¹³¹ Sasa, sulubisho la pili basi. Mtu akikubali, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,”—kanuni za imani badala ya Neno, vyeo badala ya Jina, Yeye afanyaje kwa watu? Asulubisha nguvu za Neno kwa watu. Yeye asemapo kuwa Marko 16 ilikuwa tu kwa kizazi hicho, na Mungu alisema Mwenyewe papo hapo, Yesu, akiwaambia, alisema, “Enedeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Na ihara hizi zitafuatana na hao...” Umbali upi? Kila taifa, kila imani, kila lugha, kila jamaa, kila watu, Injili ile ile. “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Na mtu anapotaribu kuondoa hilo katika Biblia, yeye asulubisha nguvu za injili kwa makutano hayo, kwa hivyo nawashtaki katika Jina la Yesu Kristo; Mna hatia ya kumuua Bwana!

¹³² Kanisa lilimchukua Yeye. Kwani? Yeye alikuwa Mungu wao hasa. Walimchukua na kumkataa kuwa Masihi wao. La, Bwana, hawakumtaka Masihi kama huyo. Na leo kanisa lafanya vivyo hivyo; lakataa Neno. Hawalitaki; Ni kinyume cha yale wamefundishwa wayaamini na kanuni zao za imani. Na Neno ndilo Masihi. Mwaamini hilo? Vema, basi kurudishwa kwa Neno ni nini? Kurudishwa kwa Masihi, ambaye ni Roho Mtakatifu kati yetu. Yeye ajirudisha Mwenyewe, ajaribu, popote Yeye awezapo kupata taa atakayoweza kupitia kwake, ambayo haijapata moshi wa kanuni za imani na kadhalika. Yeye aweze kutoa Nuru kwayo.

¹³³ Mwakumbuka wao waliamka na kutengeneza taa zao na kusafisha dohani, lakini kumechelewa zaidi. Basi mtu awaonapo hawa Walutheri, Wapresbeteria, Wamethodisti, wakijaribu kuingia katika siku hizi wapokee Roho Mtakatifu, basi, mwajua hawampati. Vema, wao waweza kunena kwa lugha na waruke juu chini, bali tazama kile kinachotendeka. Wao hakika... Ni ishara ya wakati kuwa umekwisha. Tuko katika wakati wa mwisho. Saa yoyote—Kanisa huenda likasikia wito “Njooni huku juu.” Amina! Vivyo hivyo hasa, liko tayari kabisa. Roho Mtakatifu hapa akimdhirisha Yesu Kristo kupitia wale ambao Yeye aweza kuwatumia, akijithibitisha Mwenyewe; ashuka, apigwa picha, aionyesha, afanya ishara, a—anena juu yake na kadhalika, kuthibitisha tu hasa yale yeye alisema angetenda. Akifanya hasa mambo yale yale Yeye alisema angetenda, kimaandiko. Si—au si kanuni fulani za imani wala mawazo yaliyoundwa na mwanadamu: damu nyingi, moto, na moshi na mengineyo; lakini ushuhuda wa kimaandiko (Kimasihhi).

¹³⁴ Tuna uigaji mwingi, na waigaji, na—na mengineyo, lakini yafanya tu Neno halisi ling’ae vema sana. Ndivyo. Inawafanya watu walio wa kiroho, wawezao kuamua kati ya mema na mabaya... Mwaona?

¹³⁵ Humkana Yeye. Humkana Masihi wao. “Hatukumtaka.” Jambo lile lile walitendalo leo. “Vema, kama italazimu kwenda chini kule na kutenda kama kundi hilo, siiitaki kamwe.” Vema basi, hunayo hata kidogo; hivyo tu. Waona? Vivyo hivyo leo.

¹³⁶ Ingawa Yeye alitambulishwa vyema, wao hawakumtaka Yeye, walimchukua. Mbona walimchukua? Yeye aliwaita wachungaji wao kundi la nyoka. Yeye alisema, “Enyi kundi la kuta zenye kupakwa chokaa, ninyi si kitu ila makaburi. Nje yenu imepakwa rangi kwa mavazi na kala zilizogeuzwa, na ndani ni mifupa ya wafu.” Yeye hakuwabembeleza. Maskini Mgalilaya mmoja, mwana wa seremala, lakini Yeye hakuwabembeleza; aliwakaripia.

¹³⁷ “Msidhani...” Yohana alisisima, yule mtangulizi Wake, alisema (yeye ni mwingine ambaye hakuwabembeleza), alisema, “Msije hapa mkisema mnaye baba, ndiye Ibrahimu. Mungu

aweza toka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu wana.” Naam bwana! “Shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti na kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.” Naam, bwana! Mungu ni mkali na ni thabiti na asiyecheza na Neno Lake. Naam, bwana!

¹³⁸ Tazama, Yesu, alithibitishwa kwa Maandiko... Je, mwanisikia? Yesu alitambulishwa na Mungu kwa Maandiko kuwa Yeye alikuwa ni Masihi. Sivyo? Tutaifikia shtaka la Petro katika dakika chache, nanyi mtatambua ikiwa ilikuwa hivyo au la. Yeye alitambulishwa kikamilifu, kuwa Yeye alikuwa Mungu akijidhihirisha katika Mwnadamu aliyeitwa Mwana wa Mungu. Naam. Ingawa Yeye alitambulishwa vema na kuthibitisha Neno lile la ahadi, kuwa Yeye alikuwa ni Masihi... Musa alisema, “Huyu Masihi akija, Yeye atakuwa ni nabii, na mambo haya yote yatatendeka.” Yule mwanamke akiwa na—akisimama hapo kisimani na hali hiyo yote chafu aliyokuwamo, hilo lilionyesha nini? Kuwa Mungu katika siku hizi za mwisho angewavuta wale waliotupwa.

¹³⁹ Kumbuka usiku uliopita, ile arusi—au wakati mwingine nilipohubiri hapa—ile karamu ya Arusi. Yeye alisema—jinsi alivyosema, “Nimeandaa karamu kuu na kadhalika, na watu hawa wote. Niwewaalika; na kila mmoja alitoa udhuru?”

“Sitakuja kwa maana ingeharibu kanuni zetu za imani.”

“Siwezi kuja, kwa sababu nina—mke—nimeoa mke; yeye hataniruhusu nje.”

¹⁴⁰ “Lo, ni—nilirolewa na kanisa chini hapa. Mama yangu alikuwa Mmethodisti, au Mbaptisti, au Mkatoliki, au—hata siwezi kuvumilia hilo.”

¹⁴¹ Yeye alisema, “Ninyi hamtakuja, nanyi hamtaonja karamu yangu, bali enendeni nje huko na mwashurutishe makahaba, na malaya, na walevi, na wowote walioko. Waingizeni, nami nitawaonyesha. Nimeandaa karamu yangu, na wageni wa—wangu—Meza yangu imeandaliwa; na kutakuwako na watu fulani huko.” Hawakuja; wao wanalaumu hao Wayahudi. Na leo je?

“Mimi—mimi—mimi—ni Mpresbiteria.”

“Mi—mi—mimi Mlutheri.”

“Mimi ni wa Umoja.”

“Mimi ni wa Uwili.”

“Mimi ni wa hiki; siwezi—siwezi... ”

¹⁴² Ndivyo hivyo. “Hamtakuwa huko wakati huo!” Hivyo ndivyo hasa vile Yeye alivyosema. Vema.

¹⁴³ Masihi aliyethibitishwa kabisa, Neno lililothibitishwa kabisa, lile Neno lililoahidiwa. Yule Mungu aliyeahidi Neno, kuwa hivi ndivyo Masihi angalikuwa, hapa Yeye yuaja

na kusimama hasa; Yeye aliwaambia, “Sasa, nimeshindwa wapi? Msiponiadini mimi kama Mwanadamu, aminini kazi ninazotenda, maana hizo ndizo zinaeleza Mimi ni nani. Ndizo zisemazo Mimi ndiye Masihi. Hamtaki kuniamini Mimi, maana mwadhani kuwa—kwamba yule Yusufu, pale. . . Nami nilizaliwa huko katika kibanda kidogo, na—na baba Yangu wa kambo hapa ni—seremale chini pale. Na—nanyi. . .”

¹⁴⁴ Alipoingia Galilaya, hapo, wao—naye alikuwa aenda kufanya—alisema, “He, ni nani mtu huyu? Ni nani huyu? Vema, huyu—mtu huyu, si yule ni, je, si Yose na wengineo, ndugu zake; hapa? Je, si dada zake wako pamoja nasi? Je si mama yake anaitwa Mariamu na baba yake anaitwa Yusufu? M—mlimpata wapi mtu kama huyo? Yeye alitoka kwa shule gani? Yeye hana kadi ya ushirika; yeye—yeye hana vitambulisho. Mtu kama huyo alitoka wapi. . . Haidhuru, mlimpata huyu wapi?” Na Biblia ilisema Yeye alikuwa—Yeye alichukizwa. Yeye alisema hangetenda kazi nyingi kuu, na akawaelekezea kisogo na kuondoka kwao. Yeye alisema, “Nabii hana heshima kati ya watu wake mwenyewe (mwaona?), katika nchi yake mwenyewe (tazama!)—au nchi yake mwenyewe.”

¹⁴⁵ Ndiye huyo Masihi aliyethibitshwa kikamilifu. Hakujisifu Mwenyewe; Yeye alisema, “Siwezi kufanya chochote ila kile nionacho Baba akitenda.” Na aliwahimiza waulize ikiwa huyo alikuwa Masihi.

¹⁴⁶ Na mtazame yule mwanamke mwenye sifa mbaya, yeye alilitambua. Yeye—yeye hakupotoshwa. Ile—taa. . . Yeye alikosea kwa tabia. Hakika hakuna yeyote angeliunga hilo mkono. Sheria ya Mungu imekataza hilo. Yeye alikosea kwa tabia, lakini yeye. . . Unaona, Mungu hakuhukumumu kulingana na jinsi ulivyo. Yeye—Yeye anakuhukumumu si jinsi ulivyo mkuu ama jinsi ulivyo mdogo; Yeye huhukumia moyo wako; jinsi unavyotaka kuwa. Naye hakuutaka upuzi wowote huo ulioangazwa mbele yake; hivyo ndivyo alivyotaka. Haijalishi yeye alikuwa vipi wakati huo, alikuwa tayari kuja. Mungu hukuhukumia moyo, mwanadamu huhukumia kuonekana kwa nje. Mungu huutazama moyo. Haijalishi Yeye alikuwa vipi, Nuru hiyo ilianga na hilo lilitosha. Yeye alipata kiini cha Uzima wa Milele.

¹⁴⁷ Jamani, hili ni kuu vipi kwangu (mwaona?) kuona na kujua kuwa hiyo ni kweli. Nita—nitashikilia hili. Ni. . . Hebu. . . Mungu aliye Mbinguni atainuka, na sauti yangu itakuwa katika kanda za sumaku za wakati mkuu wa Mungu huko ng’ambo. Na itahukumia kizazi hiki katika siku ya mwisho kwa sababu iko katika kanda za sumaku kisha itakuwa katika kanda ya milele wakati huo, hiyo ni kweli. Itahukumia kizazi hiki cha wahubiri ambao wana mfano wa utawa bali wanakataa nguvu za Neno, na dhihirisho lake lilipo limethibitishwa kikamilifu ya kwamba

Yeye yungali Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawashtaki kwa Neno la Mungu.

¹⁴⁸ Yanibidi nipate ahadi nyingine upesi, kwa sababu tunazo dakika kumi na tano hivi pekee.

¹⁴⁹ *Hapo wao...Hapo wao...Nini? Jamani! Kalvari. Wao walimsulubisha Yeye. Ya tatu: Wao walimsulubisha kwa kutotambua Neno lililoahidiwa la Mungu likidhihirishwa. Na mbona walimsulubisha Mtu huyo? Je, waweza kuwaza? Hebu nirudi nyuma kwa dakika moja hivi. Mbona watu wangemsulubisha Mtu kama huyo?*

¹⁵⁰ Kama Mariamu...Kama nilivyosoma kitabu kilichoitwa wakati mmoja *Mkuu wa Nyumba ya Daudi*...Kiliandikwa na Ingraham, Dk. Ingraham. Kitabu kizuri, ni mchezo wa kuigiza. Chadhaniwa kuwa kwa sehemu kweli ya maandiko ya kale yaliyotoka kwa mwanamke aliyeitwa Adena. Na... Yeye alikwenda Palestina toka huko—toka huko Misri, akarudi Cairo, naamini akamalize elimu yake. Naye alikuwa huko katika wakati wa—wa Kristo. Naye ilimpasa kumwandikia baba yake barua. Ni heri kama ungekichukua na kukisoma; ni—ni kizuri sana; *Mkuu Wa Nyumba ya Daudi*. Mtu yule yule aliyeandika Nguzo Ya Moto...Na toka kwa hicho Cecil De Mille alitoa *Zile Amri Kumi*.

¹⁵¹ Sasa, twaona kuwa katika kitabu hiki, huyu Adena aliandika barua. Naye alisema katika siku ya kusulubishwa kuwa Mariamu Magdalena, ambaye Yeye alimtoa pepo saba, alikimbia mbele ya umati, na kusema, “Yeye amefanyaje? Yeye amefanyaje? Kuponya tu wagonjwa na kujaribu kuwakomboa wale walio vifungoni. Ametenda nini ila mazuri? Niambieni!”

¹⁵² Na mtu fulani akamchapa kofi hata karibu kumwangusha huko uwanjani, na kusema, “Je, ungemwamini huyo mwanamke mpumbavu mbele ya kasisi wako?” Mwaona, oneni?

¹⁵³ Ndivyo hivyo. Mwaona? Je, Yeye alikuwa ametenda nini? Yeye hakutenda chochote. Mbona walimsulubisha? Kwanini? Kwanini? Kwa maana hawakutambua Yeye alikuwa yu nani. Na ni jambo lile lile leo. Wahubiri, na watu wa siku hizi, na waalimu wetu wa kisasa wamewafunza sana watu waamini kuwa huu ni uchawi, au ibilisi, au kusoma mafikira, au uvumi fulani, au kifumba macho fulani, hadi watu hawatambui kuwa ni hakikisho la lile Neno la Mungu kwa siku hii. Ni ishara ya siku za mwisho.

¹⁵⁴ Makanisa, usipokuwa wa dhehebu lao, watasema, “Haa, vema, huo ni utani tu. Hu—huo ni uvumi. Vema, watazame hapa chini *fulani* na *fulani*.” Lakini waache wakati mmoja wathibitishe kitu hiki halisi kuwa uvumi. Waacheni wakati mmoja wathibitishe kuwa si sahihi. Hawawezi. Haijapata kamwe kukosea, na haitakosea kamwe kwa sababu ni Mungu. Mwaona? Bali wao hupenda kutaja; wao hudhani, “Lo, kama

ingekuwa mtu fulani aliye na jina kuu..." Kwa sababu ni kundi ndogo ambalo limetupiliwa mbali, "Vema, tuliwafukuza watu hao kanisani mwetu. (Mwaona?) Hapo... Wao—walikuwa wakija kwa kundi letu (Mwaona?), lakini waliandamana na *hiki* na kuandamana na *kile*; na sasa mwaona, wanaelekea kwa... Vema, tazama ni nini, ni nani." Mimi sijali. Wangesema vivyo hivyo juu ya Petro, Yakobo na Yohana. "Mtu asiye na elimu, wala maarifa," walisema. Lakini iliwabidi watambue; kitu fulani kilikuwa kimetendeka tangu wakati huo. Walikuwa na Yesu. Hilo ndilo lililoleta tofauti. Mwaona?

¹⁵⁵ Wao walitenda hayo, kwa sababu hawakumjua Yeye alikuwa nani. Hawakujua kuwa thibitisho la Neno la Mungu halikuwa limesimama hapo siku hiyo... Sasa, ilikuwa hivyo siku moja na ilikuwa sawa. Ilikuwa hivyo wakati mmoja walipokuwa tu wakitii torati hizo na kadhalika. Lakini torati zile zile walizokuwa—walikuwa wakizitii, ziliwaelekeza kwa wakati ambao Yeye angekuja na awe Mtu huyu ambaye alipaswa awe. Wao walikuwa na sehemu *hii*, lakini hawakuchukua ile sehemu *nyingine*.

¹⁵⁶ Na wanatenda vivyo sasa. Wao wana kanisa nao wanamwamini Yesu Kristo, na wasema wanaamini, na mengineyo, lakini hukana saa tunayoishi! Bado wanarudisha ile mithali ya kale tena: Mwanadamu kila mara humsifu Mungu kwa ajili ya yale ametenda, akitazamia yale Yeye angetenda, na—au atatenda, na kutojali yale Yeye anatenda, na kuhukumiwa kwayo. Mwaona? Wao hudhani Mungu ni wa ajabu: jinsi Yeye alivyo mkuu; kile Yeye atakachotenda; Yeye atakuja; kutakuwa na kunyakuliwa siku fulani na kwenda nyumbani; na kukana ishara zile zile na maajabu papa hapa wakati ambapo Maandiko husema kuwa Yeye atafanya, wakosa jambo lote. "Kipofu akimwongoza kipofu," Yesu alisema, "wote wataanguka shimoni." Hebu ombeni Mungu tu afungue macho yetu katika hizi siku za mwisho. Vema.

¹⁵⁷ Sasa vivyo, wao wanatenda jambo lile lile leo; wao hukana na kumsulubisha Mungu yule yule leo kwa kutomjua. Vivyo kwa kumkana na kutenda... Kwa kukana mambo yale wanayoyatenda leo, wao hawamsulubishi Kristo tena hasa, lakini wao hukufuru Roho Mtakatifu. Na kwa kufanya hivi wao wana... Je, wao humkufuru Roho Mtakatifu vipi? Vipi—walimkufuru vipi hapo—huko nyuma? Mbona, hawangeweza kumkufuru wakati huo; Hakuwa amekuja bado. Walimwita Yesu "Beelzebuli"... Walimwita Yeye "Beelzebuli" kwa sababu Yeye angejua siri za mioyo na kadhalika. Wao walisema, "Huyu ni ibilisi." Yaani, "Yeye yu mpiga ramli. Hivyo ndivyo yeye atendavyo haya, ni kwa kupiga ramli. Yeye si kingine ila ibilisi." Mwaona, hawakuwa na nabii kwa miaka mia nne, na waliwasahau. Mwaona? Wao walikuwa tu na torati yao. Walisema, "Huyu ni Beelzebuli."

¹⁵⁸ Na Yesu alisema, “Nitawasamehe hayo, lakini Roho Mtakatifu ajapo (mwaona sasa?), nena neno moja tu dhidi Yake, na hautasamehewa hilo.” Kumbuka, itakuwa na haiwezi kwa vyo vyote vile, kuwa na huruma... Unapokufuru na kumwita Roho wa Mungu, Neno la Mungu, ambalo limethibitishwa na Roho (mwaona, Neno lasema hivyo; Roho analithibitisha), na unamwita kitu kichafu, umevuka mpaka wa rehema na hukumu na huwezi kusamehewa hilo. Hiyo ndiyo sababu nakishtaki kizazi hiki kwa kuwa na hatia ya kumsulubisha, kukufuru, Mwana wa Mungu aliyedhihirishwa! Hiyo ni ahadi Yake kwa manabii wote, na Kristo Mwenyewe katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na siku za Sodoma.

¹⁵⁹ Kukufuru, kule wanakomsulubisha Mwana wa Mungu upya kwa watu. Yeye yu Neno lililothibitishwa. Neno moja tu dhidi Yake halitasamehewa kamwe. Sasa, utafanyaje basi? Utasimama wapi? Wao wamehukumiwa, wanangoja tu saa ya kumwagwa kwa ile ghadhabu ya Mungu. Yeye atawapondaponda.

¹⁶⁰ Huyapenda mafundisho ya madhehebu ya watu na mafundisho ya sharti kuliko wapendavyo Neno lililothibitishwa la Mungu, hiki kizazi cha watu! Jamani! Ni—laiti ningalikuwa na wakati mrefu kwa hili. Kizazi hiki cha watu, “Kizazi hiki hukataa ufunuo wa Mungu, lakini tunatembea ambapo mitume walipitia.” Hiyo ni kweli. Mungu...

¹⁶¹ Mwasema, “Vema, wengine wasema hilo pia.” Mungu hulithibitisha.

¹⁶² Yesu alisema, “Ikiwa kazi hazineni kunihusu Mimi basi endelea tu na kusema ninajinenea habari Zangu Mwenyewe. Lakini kazi zanena, heri muamini kazi (mwaona) kwa sababu ndio wakati.” Akasema, “Mwajua kesho jua litang’aa au kutakuwa na dhoruba kwa maana mbingu ni nyekundu tena kumetanda; kesho kutakuwa na kianga.” Kasema, “Mwaweza kutambua uso wa anga, lakini ishara za wakati hamjui lolote kuzihusu. Mngalimjua Mungu, mngaliujua siku Yangu.”

¹⁶³ Wao wakasema, “Unajichukulia mengi, unajifanya mwenyewe Mungu.” Nao wakamwangika msalabani.

¹⁶⁴ Na Roho Mtakatifu leo sio nafsi ya tatu; Ni Mungu Mwenyewe, aliyedhihirishwa katika mwili wa mwanadamu kwa Damu ya Yesu Kristo kutakasa maisha apate kujirudisha mwenyewe kwake. Nao wanasulubisha Neno lile lile lililodhihirishwa. Mwaelewa? Kusulubiwa kwa Kristo leo ni watu watakaokataa Mwana wa Mungu aliyethibitishwa na kudhihirishwa miongoni mwa watu kwa mambo Yake aliyosema yangetukia katika siku za mwisho kwa Neno Lake. Mwaona?

¹⁶⁵ Sasa, thibitisho lile lile lapaswa liwe lile lile ikiwa Yeye yu Mwana yule yule wa Mungu, kwa sababu Yeye alisema katika Yohana 14:12 sasa, kuwa, “Kazi nizifanyazo mimi, nanyi mtazifanya,” Waebrania 13:8: “Ni yeye yule jana, leo na hata

milele.” “Na mkikaa ndani Yangu... (Yohana 15) Ninyi mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni tu lote mtakalo nanyi mtatendewa.” Naam, bwana!

¹⁶⁶ Kumbuka, wao walikuwa watu wa kidini mno waliotenda hilo. Hawakuwa watu wa nje. Walikuwa watu wa kidini wa siku hiyo. Na hao wanaoyafanya hayo leo ni watu wa Kidini. Sulubisho lile lile, jambo lile lile siku hizi.

¹⁶⁷ Upesi. *Hapo wao walimsulubisha Yeye.* Wakati huo? Hakika. Ndipo wao walikuwa wakikana Neno la Mungu lililodhihirishwa, wakikubali kanuni zao za imani badala ya lile Neno. Si hilo ndilo wanalofanya siku hizi? Ndivyo hasa, wanatenda yale yale leo. Yeye alikuwa Neno, na wao walikataa lile Neno. Hilo ndilo jambo moja nataka msilikose, nataka msilikose. Yeye alikuwa Neno na walipomkataa, walilikataa Neno. Nao walipomkataa, mwishowe walimsulubisha. Na hivyo ndiyo wamefanya leo; kukataa Neno la Mungu, na kukubali kanuni za imani yao, na wameisulubisha hadharani, mbele ya makutano yao, kazi ya Roho Mtakatifu. Nao wana hatia, nami nawashtaki katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁶⁸ Kwa miaka kumi na mitano nimemwona Yeye akienda kote duniani, na hali wao wangali wanashikilia kanuni zao za imani. Wana hatia! Wao walilichukua lile Neno ambalo lingelea kanisa—makanisa yote pamoja na kuunda umoja mkuu wa kindugu kati ya Wapentekoste na wengine wao... Badala ya kufanya hivyo, wao walilikataa, na kulitupilia mbali, na wamelifanyia mzaha, na kuliita kila kitu sasa; na sasa kwa muungano wa kanisa, kupitia kwa mpango wa ibilisi, wajaribu kuingia na kusema, “Sasa tutakuja tununue mafuta.” Wao wamekataliwa leo. Wana hatia ya kumsulubisha Yesu Kristo. Yachukue kwa masharti ya Mungu au... Masharti yako hayawezi kufanya kazi. Mwaona?

¹⁶⁹ Wao walilikataa Neno la Mungu lililodhihirishwa, kwa ajili ya kanuni za imani zao, nao wanatenda lile lile leo. Yeye alikuwa ni Neno, Injili ya Yohana 1. Waebrania 13:8 yasema ni Yeye yule jana, leo na hata milele.

¹⁷⁰ Sasa, wao wanamsulubisha upya. Je, wajua Biblia ilisema tungetenda hivyo? Ni wangapi wangependa kusoma kidogo? Je, mngeniongeza tena dakika kumi na tano? Vema! Hebu tufungue kwa dakika moja hivi... Kumsulubisha Upya. Hebu tufungue Waebrania sura ya 6 na tusome kidogo, Waebrania sita, na tuone ikiwa twamsulubisha Mwana wa Mungu upya. Tuone kama yaweza kutendeka. Mwasema, “Huwezi kumsulubisha tena mara ya pili.” Tutaona ikiwa twaweza au la. Neno la Mungu ni kweli. Sivyo? Waebrania 6:1

Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;

tusiweke...msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu.

Na wa mafundisho ya ubatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele.

...haya tutayafanya Mungu akitujalia.

¹⁷¹ Mwaona? Paulo ataka ijulikane kuwa mambo haya ni muhimu sana: mabatizo, kuwekea mikono, na kufufuliwa, kuja kwa pili. Mambo haya yote ni ya milele; haya ni Kweli hasa. Sasa tazama!

Kwa maana...(Someni nami—kifungu kimoja tu. Nataka ninyi msome nami sasa, kifungu cha 4:)

Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu.

Na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,

Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.

¹⁷² Sasa, je, hilo ni Neno langu au Lake? Mtu aliyepewa nuru... kumbuka, hawakuipata; wao walikuwa waumini waliokwamia mpakani. Baada ya sisi kupokea nuru ya Neno la Mungu (unaipata toka kwa maarifa tokana na kulisoma na kulifahamu) ndiposa ukilikataa, basi u—haiwezekani kwako kuokolewa! Je, umesoma hilo sasa? Waona? waliokwisha kupewa nuru... Waifahamu tu, hukuipata.

¹⁷³ Ni kama hao waumini waliokwenda... Ni mfano halisi wa safari. Huku—huku—huku kutoka kwa tatu ni mfano tu wa kwingine kwote.

¹⁷⁴ Tazama! Tazama nyuma huko. Hebu nikuonyeshe kitu fulani sasa kwa dakika moja hivi. Samahani kwa msemu. Tazama! Israeli waliwachukua watu kumi na wawili, mmoja kwa kila kabila, viongozi wa kimadhehebu, na kuwapeleka hadi ukingoni mwa mpaka, nchi ya ahadi, na kuwaonyesha wao mambo mema yatakayokuja, walichokuwa nacho. Na walirudi nyuma wakilalamika kuwa, “Hatukuweza kulifanya.” Lakini kulikuwa na wawili kati ya hao kumi na wawili; Yoshua na Kalebu walisema (wao walilitazama Neno), “Mungu alisema ni yetu, nasi twaweza kuitwaa bila shaka.” Sivyoy?

¹⁷⁵ Hiyo ilikuwa ni nini? Waumini waliokwamia mpakani. Mwaona? Wao hakika walizaliwa kanisani. Walikuwa viongozi wa watu; wao walikuwa maaskofu tuseme. Hao waliotembea pale Neno la Mungu lilipoonyeshwa kuwa Kweli. Kuna nchi; wao hawakuwa wamefika huko. Hawakujua ilikuwako. Lakini wao walishuka kuona ilikuwako. Ilikuwa pale. Na Kalebu na

Yoshua walikwenda ng'ambo, na kuleta ki—ki—kichala cha zabibu, na kuwaruhusu wale baadhi yake; nao walionja ya nchi nzuri na ndipo wakarudi nyuma na kusema, "Hatuwezi kuitwaa. (Mwaona?) Hatuwezi kulitenda."

¹⁷⁶ Hapa mna kundi lile lile katika wakati wa Yesu Kristo: "Rabi, twajua kuwa wewe u mwalimu uliyetoka kwa Mungu." Mwaona? Mkwamia mpakani. "Twajua wewe u mwalimu toka kwa Mungu. Hakuna mtu awezaye kufanya mambo haya ufanyayo. Twatambua kuwa Mungu yuko." Mbona hawakulipokea? Mbona hawakulichukua? Wakwamia mpakani, wakwamia mpakani.

¹⁷⁷ Wako hapa kwa huku kutoka kwa tatu; ishara ile ile, dhihirisho lile lile, Kristo yule yule, Roho Mtakatifu yule yule, kazi zile zile. Mungu yule yule, Ujumbe ule ule, nao hawawezi kuupokea. Ingewabidi waache kadi zao za ushirika.

¹⁷⁸ Ni nini? Wamekwisha kupokea nuru. Wao walitazama na kuona ni kweli hasa. Hawawezi kulikana. Magazeti yameshuhudia wameliona. Picha, magazeti, ushuhuda, ufufuo wa wafu, hati za thibitisho za wagonjwa toka kwa madaktari: yawabidi waseme huyu Ndiye. Na utabiri, hakuna hata mmoja wao umekosa kutimia katika miaka hii yote, kila mmoja wao hasa kwa kila jambo, hawawezi kusema cho chote ila tu kuwa ni Mungu. Lakini hawawezi kulikubali.

¹⁷⁹ Hilo kundi la wahudumu huko Chicago, mia tatu na kitu wao walikuwa waje na wabatizwe katika Jina la Yesu Kristo. Wao wako wapi? Gharama ni kubwa sana. Hawawezi kufanya hivyo. Ni nini? Biblia ilisema wafanyapo hilo... Wao hufanyaje? Wajitenga wenyewe na neema wakaingia hukumuni, "Maana haiwezekani kwa wale waliopewa nuru (wameshaletwa kuitazama), na wamekwisha kupokea nuru na wameonja Neno zuri la Mungu;" wakiliacha, ambapo itawabidi kujifanya upya tena, kusema, "Vema sasa, nitafanya! Naam!"...

¹⁸⁰ Enyi Wapresbiteria, enyi Wamethodisti, na Wabatisti, na Walutheri, na huu upuzi wa Wafanyi Biashara wa Injili Nzima, wanaosema wanaingia, wameukataa huu Ujumbe. Kanisa lako lita... Ikiwa kuna watu binafsi ndani humo, hakika, lakini si kanisa. Yakubidi uondoke kanisani ili uupate. Unaona? Ndivyo. Watu binafsi waweza.

¹⁸¹ Lakini unapodhani kanisa la Presbiteria litapokea Roho Mtakatifu, nao wote wanapeleka hati zao...? Daima usiwaze hilo! Nanyi mwadhani ninyi Wamethodisti mtafanya hivyo? Ninyi hamtafanya kamwe. Je, mwadhani ninyi waumini wa utatu mtapokea Jina la Yesu Kristo na mbatizwe kila mmoja wenu katika...? Hamtalitenda kamwe; hamtalitenda kamwe. Lakini watu binafsi wataondoka na kulitenda. Naam. Na hiyo ni ishara ya kuja Kwake! Lakini hayo makanisa yaliyoona Kweli na kuikataa katika mabaraza yao, haiwezekani... Basi wao wana

hatia ya kumsulubisha Yesu Kristo. Nami nawashtaki wao kwa Neno la Mungu, ya kuwa Mungu ame. . .

¹⁸² “Je, unawashitaki vipi, Ndugu Branham?” Nawashtaki, kuwa Mungu amejitambulisha Mwenyewe dhahiri katika Neno Lake siku za mwisho, na kujijulisha Mwenyewe kuwa ni Yeye yule jana, leo na hata milele, na wameitupilia mbali. Na mna hatia ya kumsulubisha Yesu Kristo, kwa kumkufuru Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

¹⁸³ Twawapelekeni kwa Waebrania 10. Tena, ambapo yatwambia tena katika Maandiko, si kuwa tu haiwezekani, lakini hamwezi kamwe. . . Yawatenga ninyi milele toka kwa Mungu. Hamwezi kuja katika Uwepo a Mungu tena mnapomkataa Roho Mtakatifu na kumdhihaki.

¹⁸⁴ Sasa, oneni? Umelionja Neno. Oneni? Waumini wakwamia mpakani. “Lo,” mwasema, “hao watu hawakuwa waumini.” Wao walikuwa waumini au walidai kuwa waumini, lakini ijapo kwa Neno. . . Walikuwa Israeli; waliondoka kupitia kwa damu. Waliondoka chini ya ishara ya Musa; walikuwa wameona ishara hizo zikitendeka.

¹⁸⁵ Mungu alisema, “Nitawapeleka huko ng’ambo.”

¹⁸⁶ Ilipofikia jambo muhimu la Neno lililoahidiwa kuwa litakuja, wao wangesemaje? “Ah, hatuwezi kulifanya.” Mwaona? Na hapa wao walirudi na zabibu na kila kitu kudhihirisha kuwa nchi ikuwa nzuri. Neno la Mungu ni kweli.

¹⁸⁷ Mungu alisema, “Nitawapeni —lakini yale mazingira!

¹⁸⁸ “Lo,” Kasema, “Twaonekana kama panzi kando yao. Hatuwezi kulifanya.” Haijalishi vipi. . .

¹⁸⁹ Miaka michache iliyopita wakati hiki kibanda kikuukuu kilikuwa hapa kama maskani, mtu fulani aliingia, akaondoka nje hapo, na kunizungumzia na kusema, “Billy, utahubiria vizingiti vinne siku moja hivi karibuni kwa ujumbe kama huo.”

¹⁹⁰ Nilisema, “Nitahubiria vizingiti vinne, maana Mungu aweza kumwinulia Ibrahimu watoto toka kwa hivi vizingiti.” Ndivyo; ni kweli. Nilisema, “Ikiwa una jambo fulani ambalo unaweza kuthibitisha kuwa si kweli, tueleze.” Ni jambo moja kuwika-wika, lakini iwapo ni kuthibitisha, hayo ni tofauti. Naam! Hiyo ndiyo huleta tofauti. Vema.

¹⁹¹ Hapa kwa hizo kanuni za imani wao wamemsulunisha Yeye upya. Sasa, Waebrania sura ya 6, tukiendelea chini. Tungesoma tu kuendelea, kote mpaka hapa. Tuna wakati mwingi. Niliandika kifungu fulani hapa, pale itakuwa (Waebrania sura ya 6, tu—nadhani, tuisome yote) haiwezekani kwa wale waliopewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu. . . Hatuna wakati mrefu uliobaki, maana nina Andiko lingine nataka ninyi mlisome kwa muda mfupi.

¹⁹² Tazama hili! Wao wenyewe wanamsulubisha Mwana wa Mungu upya. Wao walifanyaje? Nini? Kwa kuwa na muonjo na kujua kuwa ni Kweli, na kisha wageuke na kulikana, Je, wao hufanyaje? Haiwezekani. . .

¹⁹³ Kwa hivyo ndivyo hili taifa limetenda. Hivyo ndivyo watu hawa wametenda. Hivyo ndivyo makanisa haya yametenda. Wamelikataa, nao wamesulubisha Ujumbe huu; wamesulubisha Kweli kwa watu. Walimfanyiaje Yesu? Walimfedhehi, walimvua nguo Zake, na kumwangika msalabani, na kumpigilia misumari juu hapo, yule mkuu wa Uzima. Wamefanya jambo lile lile leo kwa kanuni zao za imani. Wao wametenda jambo lile lile. Wameyavua mambo; wameuvua ule uzuri, na mavazi ya Injili kwa kujaribu kuiweka mahali pengine, na kumwangika Yeye msalabani. Lo, mie! Kwa nini?

¹⁹⁴ *Hapo wao—hapo wao walimsulubisha. . .* Sasa, fungu la kunukuuliwa la mwisho. *Yeye, Yeye*, huyu Mtu wa thamani sana. Mbona walifanya hivyo? Hawakumjua Yeye. Mbona wanalitenda leo? Hawajui hii ni Kweli. Wana—wao ni bubu na vipofu kwa hayo. Hawajui; hiyo ndiyo sababu. Kanuni za imani zao na mapokeo yamewapeleka mbali na Neno la Mungu.

¹⁹⁵ Sasa kwenu hapa, katika kufunga sasa, sikilizeni kwa makini. Mwaona? Najua kuna joto; pia nina joto. Lakini, ee, ndugu, Neno hili, ni Uzima ukilishikilia. Tazama! Si kitu fulani tunachokinena ambacho labda kitatendeka baadaye. Ni kitu ambacho tayari kipo hapa pamoja nasi na kinatendeka sasa, si kitu ambacho kitakuwepo, kitu kilichoko. Hatushuhudii, “Twajua kile Yeye ametenda; twajua kile Yeye atakachotenda,” lakini sasa, twanena kile Yeye anachotenda. Mwaona? Huu ndio wakati wetu. Labda hatuwezi kuishi tuone kule kunyakuliwa. Labda naweza kufa leo; wewe waweza kufa leo. Sijui. Lakini kunyakuliwa kunakuja; huko ni—huko ni. . . Huko kujapo, tutakuwa huko; msifadhaike, ndivyo wengine wao watakavyokuwa, kote toka kule nyuma katika zile nyakati zote ambapo wamekuamini, na kukutazamia. Wao walitembea katika nuru ya siku yao, na Nuru hiyo ndiyo hii. Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo na hata milele. Acheni kanuni zenu za imani na muamini Neno hili. Hili ni Kweli; Neno ni Kweli. Yesu alisema, “Neno Langu ni Roho, Neno Langu ni Uzima.” Utapokeaje uzima ukiukataa Uzima? Utaingizaje fundisho la sharti ambalo ni mauti, na Neno la Uzima? Je, ulitupilie mbali Neno la Uzima uchukue mauti? Utapokeaje hayo mawili kwa wakati mmoja? Huwezi kufanya hivyo. Na kila neno la mwanadamu liwe uwongo, kila fundisho la sharti uwongo; Neno la Mungu ndilo Kweli.

¹⁹⁶ Nahimiza mtu aweye yote anionyesha mtu yeyote (nami najua kanda hii inaenda ulimwenguni kote), mtu yeyote, askofu yeyote, atakayekuja nisomeapo au mbele ya makutano haya na kuonyesha mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi

kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu katika Agano Jipya. Nitawaonyesha ambapo kila mtu aliyewahi kubatizwa, na wale wote waliobatizwa vingine iliwabidi wabatizwe tena ili wampokee Roho Mtakatifu. Je utafanyaje kuhusu hilo? Je, ukae huko nje kwa kanuni zako za imani? Ukae huko nje katika mafundisho yenu ya sharti na kufa! Mna hatia, mikono miovu, mmemchukua yule Mkuu wa Uzima, Neno la Uzima, na kulisulubisha mbele ya watu.

¹⁹⁷ Sasa, wao walifanyaje? Hawakuijua. Siku hizi watu hutembea kwa kutokujua, hawajui hiyo ni kweli. Wanadhani ni aina fulani ya dini. Hawachimbui chini kutosha waingie katika roho ya ufunu. Hawaombi kutosha; hawamlili Mungu kutosha. Wanaichukua kijuujuu tu, “Ah, vema, naamini ni Mungu. Hakika!” Ibilisi anaamini jambo lile lile. Ibilisi analiamini zaidi ya watu wengine wanavyodai wanaamini; ibilisi analiamini na kutetemeka. Watu wanaliamini tu na kuendelea, lakini ibilisi hutetemeka, akijua hukumu yake inakuja. Na watu wanaliamini na hawajali hukumu inayokuja.

¹⁹⁸ Hatia ya kumsulubisha Yeye. Hakika! Nakishtaki kizazi hiki, nawapata na hatia kwa Neno lile lile lililowapata na hatia mwanzoni. Hiyo ni kweli. Yesu alisema, “Ni nani aweza kunihukumu Mimi?” Yeye alikuwa Neno lililofanyika mwili. Na leo Neno lile lile limefanyika mwili.

¹⁹⁹ Petro alisema katika shtaka lake katika Matendo... Hebu tulisome. Petro, alipoyaona haya yakitendeka, kile wametenda, yule Roho... Tazama, Petro alikuwa akimtetea Kristo, kile walikuwa wamemtendea. Natetea kile Injili zilicho. Na... Petro alikuwa akiwashtaki kwa kumwua Mtu, Kristo, aliyekuwa Neno. Nakishtaki kizazi hiki kwa kujaribu kuliua Neno lililofanyika mwili katika mtu. Tazama kile Petro alichosema. Lazima hasira yake ya haki ilizidi sana. Msikize hapa katika Matendo sura ya 2 na anzia na kile kifungu cha 22.

Enyi wanaume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, aliyedhihirishwa—mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza... na ma ajabu na ishara ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati—yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua.

²⁰⁰ Whiuu! Waza wao walivyojisikia! Sikiza hilo.

²⁰¹ Enyi wanaume wa Israeli,... Yule mkuu, enyi watu wa Kanisa, ninyi watu watakatifu, ninyi makasisi, ninyi wanaume mnaodhaniwa kuwa watu wa Mungu, sikizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti alidhihirishwa na Mungu kwenu.

²⁰² Sasa, nawaambieni ninyi wahudumu na ninyi watu, Yesu wa Nazareti, Roho Mtakatifu, Yeye yuko huku katika Utu wa Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa Uzima uliokuwa ndani Yake. Yeye yuko hapa akitenda kupitia kwa watu na kujidhihirisha

Mwenyewe kwa ishara na maajabu ambayo Yeye anatenda. Na hapa wao wameweka ukutani utambulisho wa kisayansi. Na watu wanaketi hapa waliokuwa wamekufa na wanaishi leo; na walioliwa na kansa, nao wana afya leo. Vipofu wanaona leo, viwete wanaotembea leo! Yeye ni Yesu wa Nazareti.

Mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, . . . (aliyechaguliwa tangu asili kwa kazi Yake) . . . ninyi mkasulubisha kwa mikono ya watu wabaya . . . mkamwua;

203 Hilo—hilo ni shtaka? Yeye anashtaki nini? Hilo baraza kuu la Kiyahudi. Nami nashtaki, asubuhi hii, muungamo wa makanisa; nawashtaki Wapentekoste; nawashtaki Wapresbiteria, Wabatisti, na kila dhehebu ulimwenguni. Kwa uovu, uchoyo wa pupa mmelichukua Neno la Uzima na kulisulubisha mbele ya watu, na kulikufuru, na kuliita kurukwa na akili ambalo Mungu aliinua kati yetu kuthibitisha kuwa Yeye ni yule jana, leo na hata milele. Nakishtaki kizazi hiki!

204 Mungu amejithibitisha Mwenyewe kuwa hai. Mungu amethibitisha kuwa hili ni Neno Lake. Mna nini ila tita la mafundisho ya sharti na kanuni za imani? Mwaweza kuonyesha ni wapi alipo Mungu aishiye? Kwa maana mmelikataa Neno la Uzima ambalo lingewapa mambo haya. Naam, bwana! Jamani, wakati jinsi gani tunaoishi sasa. Whiuu! sawa . . .

205 Oh, naita . . . Petro alisema, “Mmemchukua kwa mikono ya watu wabaya mkamsulubisha na kumwua:”

Ambaye Mungu . . . alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.

206 Na kwa kanuni zenu za imani, na miungano yenu, na madhehebu yenu yaliyo na mfano wa utauwa . . . ? . . . mifano yenu ya utauwa, mmekataa nguvu za kufufuka Kwake. Lakini saa imefika; siku za mwisho ziko hapa, ambapo Mungu aliahidi kulingana na Malaika 4 kwamba Yeye angeinuka katika siku za mwisho na angeigeuza mioyo ya watu ielekee baraka za asili na imani ya baba wa Kipentekoste. Na hamwezi kuikana, na hamwezi kuizuiwa. Na sasa, nawahukumu ninyi, mna hatia, na nawahimiza, na kuwashtaki mbele za Mungu, ya kwamba kwa mikono ya kidhehebu ya watu wabaya na wachoyo mmesulubisha Neno la Mungu mbele za watu. Nami nawaita wenye hatia na tayari kuhukumiwa. Amina. Naam, bwana!

207 Natoa wito ule ule ambao Petro aliutoa. Yeye alitoa wito kwa kizazi hicho kutubu. Natoa wito kwa kizazi hiki kutubu wamwelekee Mungu na kurudia Kweli ya asili ya Neno. Rudieni ile imani ya baba zetu. Rudieni Roho Mtakatifu, maana Mungu hawezi kulibadili. Mungu aliposema, “Ishara hizi zitafuatana hao waaminio,” Yeye yabidi alishikilie hilo milele; ni Neno Lake.

208 Msemapo, “Salimianeni kwa mikono,” au “Pokeeni ushirika,” au kitu kama hicho, au chochote kwa kanuni hizo za imani, au kitu fulani cha wazo kama hilo; ambacho mtu yeyote; mlevi yeyote asiyeamini yeyote aweza kukifanya, mwigaji yeyote, au kahaba yeyote aweza kufanya hicho; kupokea ushirika, kuwa na taratibu, na kadhalika; ungeweza kulitenda. Lakini Yesu alisema hii ingekuwa kitambulisho: “Ishara hizi zita (si labda, zitafuatana)...katika vizazi vyote kwao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha nzingine, wanene kwa lugha mpya; na kushika nyoka; kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Ponya wagonjwa; fufua wafu; toa pepo, mmepokea bure, toeni bure.”

209 Na mipango hii yote ya kupata pesa na mengineyo imenasa vitu vyote leo, si ajabu wamejawa sana na hukumu. Naam, bwana! Oh, mie!

210 Hebu tuone sasa. Naam, bwana! Wito wa toba. Na kushtaki kwangu sasa...Hii Kalvari mpya ni—ni kanisa, inayoitwa patakatifu sana, mimbara mikuu, madhabahu ya katoliki, madhabahu ya Katoliki, inayoitwa mimbara yao. Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteria, Walutheri, Wapentekoste, mahali patakatifu sana hapo, hapo Yeye hupata michomo Yake mikali sana—Kalvari mpya. Inapatikana wapi? Katika mahali patakatifu, kanisani. Yeye amesulubishiwa wapi? Toka kwa wachungaji. Enyi wanafiki, mwajua vema zaidi ya hilo! Sina hasira, lakini kitu fulani ndani yangu kinachochea. Mungu ametambulikana vema sana kati yenu.

211 Yeye alipata wapi mikuki hii ubavuni Mwake? Alipata wapi michomo yake? Kalvari. Yeye anaipata wapi leo? Mimbarani. Ilitoka wapi? Yerusalemu. Inatoka wapi? Madhehebuni, wale waliodai wanampenda, hao ndio waliomchoma. Ndio wamchomao siku hizi. Kalvari Yake ya pili, ambapo Yeye apokea michomo Yake dhidi ya Neno...Hiyo ndiyo inayomchoma. Yeye yu nani? Yeye yu Neno. Yeye ndiye Neno. Yeye amechomwa sana toka wapi? Mimbarani katika mahali palipo patakatifu, kama tu ilivyokuwa wakati huo.

212 Nina haki ya kushtaki kizazi hiki. Nina haki ya kufanya hivyo kama mhudumu wa Injili ya Yesu Kristo pamoja na ishara hizi kuu na kuthibitisha kuwa Yeye yu Mungu. Nina haki ya kuleta shtaka dhiki ya kizazi hiki, maana makali ya mkuki yametoka hapo mimbarani, ambapo wamelilaumu na kusema, “Msiende huko kusikiza upuzi huo. Hayo ni ya ibilisi.” Papo hapo mahali ambapo anapaswa kupendwa.

213 Na ishara zile ambazo Yesu alisema zingetendeka...Neno la Mungu li kali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili (lile Neno), hupambanua nia na makusudi ya moyo; na linaitwa shetani. Toka wapi? Mimbarani, mahali patakatifu. Ee, Mungu,

aweza je kutazama chini? Ni—ni huruma tu, hivyo tu, neema. Hatuwezi kutenda chochote ila kuelekea hukumuni. Tayari tuko hapo.

²¹⁴ Liwazie. Michomo Yake mikali huja toka mimbarani. Hapo ndipo Kalvari Yake ilipo. Wao humsulubisha, yule Neno, mimbarani. Hiyo ni kweli. Vipi? Wanalifanyaje? Kwa mifano yao ya utauwa. Ndivyo hasa!

²¹⁵ Kavikwa taji, na wasikilizaji, wenye kudhihaki; Yeye ana taji mpya ya miiba. Wenye kudhihaki humchoma toka mibarani, huvikwa taji na wadhihaki.

²¹⁶ Amesulubishwa tena upya? Amevuliwa nguo kwa kanuni za imani zilizotengenezwa na wanadamu, waalimu wa dhehebu hupinga Neno Lake. Wao hulivua, kwa fedheha, wao hulilaumu.

²¹⁷ Yesu alisema, “Wao huniabudu bure.” Bure. Haifai kitu. Wao humwabudu nani? Humwabudu Mungu yule yule. Walikuwa wakimwabudu Mungu yule yule katika kusulubiwa Kwake kwa kwanza, na kulikuwa kuabudu bure. Ndivyo ilivyo siku hizi. Walijenga madhehebu haya bure. Wanajenga seminari hizi bure. Wana kanuni hizi za imani bure, wakifundisha maagizo ya wanadamu na kulikataa Neno la Mungu. Wao wana hatia ya kumsulubisha yule Mkuu wa Uzima, wakifundisha mafundisho ya mwanadamu badala ya Neno Lake. “Wao huniabudu bure”—amevuliwa nguo, kuchomwa na kuvikwa taji.

²¹⁸ Mnapomwona huyo akielekea katika barabara ya mji... Nanyi wanawake wengine mlio na nywele ndefu... Mwasema, “Yeye ni wa mtindo wa kikale, sivyo?” Kumbuka, huyo ni mwenye dhihaka. Hiyo ni taji unayovaa. Mungu alisema ni utukufu wako. Ivae kwa ujasiri. Haleluya! Ivae kwa fahari, kama vile ungevaa taji ya miiba kwa ajili ya Bwana wako, ivae kwa fahari! Usiaibike. Yeye alisema hivyo. Haijalishi hawa Yezebeli wasemaje leo, yale hawa walaghai wanaosimama mimbarani, wamsulubishao Kristo, haijalishi wao wasemaje, ivae kwa fahari. Mungu alisema hivyo. Itunze tu.

²¹⁹ Amevikwa taji na wenye dhihaka tena, miiba; anachomwa toka mimbarani pamoja na kanuni za imani.

²²⁰ Yeye amepata Golgotha mpya. Je, wao walimpeleka wapi?

²²¹ Hawa waimbaji waliovaa majoho, wanawake wavaa suruali fupi, waliofupisha nywele, waliopaka nyuso rangi, wakiimba vizuri sana katika kwaya kama malaika, hiyo ni Golgotha Yake mpya: katika tu kule kujivua nguo uchi hadharani kwa kisasa, ambako kwalindwa na sheria kama ilivyokuwa Sodoma na Gomara.

²²² Mwaona mbwa jike akitembea katika barabara ya mji, wakati fulani hakuna hata mbwa dume mmoja atakayemjongelea. Acha kitu fulani kitendeke na kila mbwa dume atamwendea yule jike. Kuna kitu fulani kimetendeke

kwake; mwajua sababu yake. Hebu... Mbona wanawake hawa wanavua nguo zao na kutembea katika barabara za mji? Usiniambie si kitu kile kile. Ni utambulisho. Usimlaumu huyo mwanamume. Lakini wao wanalindwa na sheria ya Sodoma. Sheria hiyo... Nasema ni—si halali kwao kuwa nje huko. Na wahubiri mimbarani wanapaswa kuvalia kamisi badala ya joho la kikasisi. Wakisimama nje hapo na wataliruhusu, na waona haya kulipinga, kwa maana dhehebu lao litawafukuza, mwasulubisha Neno la Mungu kwa—kwa makutano ambalo lasema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa mavazi ya mwanamume. Nalaumu jambo hilo. Nakishtaki kwa kusulubisha Neno la Mungu mbele ya watu. Wanawake waliofupisha nywele, wanaovaa suruali fupi hadharani, wasimama katika kwaya.

Mtu fulani aliniambia hivi majuzi, mwanamke fulani aliniuliza, alisema, “Wapi—wafikiri watapatikana wapi?”

²²³ Nilisema, “Kama Bwana akiniambia kutafuta dazan moja ulimwenguni, ninge—ningefadhaika sana.” Wakati wa kupambanua kwa Roho, husimama hapo na kuwatazama; wao husimama vile, na kuyaona mambo yaliyo juu yao, wachafu, waovu, wavuta-sigara nje hapo, wakiendelea hivyo, na kusimama katika kwaya zenye majoho na kuimba katika hali hiyo, na kuacha wasikizaji wawaone kama... “Vema kama yeye aweza kuimba, mimi pia naweza.”

²²⁴ Maisha ya Kikristo ni maisha ya utakatifu, usafi, mhudumu. Nawashtaki katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya uovu na uchafu wao. Wameifedhehi Injili. Na wao wanaojaribu kuitii wanaitwa waliorukwa na akili. Huitwa “Hao ni wa mtindo wa kale.” Upunzi!. Nawashtaki katika Jina la Yesu Kristo.

²²⁵ Wanawake waliojivua nguo wa kisasa wako barabarani, huimba katika kwaya, huvuta sigara, hufanya mizaha michafu, wamekuwa na waume watatu au wanne na wanamtafuta wa sita, ndiposa kujiunga na kwaya kwa sababu wana sauti... Enyi wanaelimu fukara, mliopungukiwa kiroho, mmekataliwa kwa msimamo wenu wenyewe, mwaisoma Biblia ile ile ambayo mtu mwingine yeyote aweza kusoma; lakini mmekataa Roho wa Mungu, hata Biblia ilisema mngeletewa nguvu ya upotevu, muuamini uongo ili mhukumiwe kwa huo! Ninyi hakika mwaamini kuwa mu sahihi, na Biblia yasema mngeuamini na kuangamizwa na uwongo uo huo ambao mnaamini kuwa ni kweli. Hivyo basi nawashtaki ninyi kwa Neno la Mungu. Mnawafundisha watu kosa na kusulubisha kanuni za Kristo, za utakatifu, na Uzima utokao juu.

²²⁶ Mtu fulani aweza kutembea kwenye barabara ya mji na kuwa mtu tofauti. Wahubiri wakisimama kwenye viwanja vya mpira wakivuta sigara—mawe ya kujikwaza. Na mengine hayo yote maovu wanayovumilia. Wanawake katika kwaya zao,

wakivaa suruali fupi, wamefupisha nywele, na kuendelea vivyo hivyo, wamejipaka rangi nyusoni, na ndipo wawaite, “Dada *fulani* na *fulani*”; na Biblia inalauumu upuzi huo! Hiyo ni kweli. Wanaenda kwa karamu na kufanya yasiyofaa, bado angali mshiriki wa kanisa, shikilia ushuhuda wako na uishi vyo vyote utakavyo. . .

227 Msidhani nanena haya yote kuhusu Wapresbiteria; nanena kuhusu ninyi Wapentekoste! Hiyo ni kweli. Ninyi wakati mmoja mlijua Kweli, lakini mlidhani hamngeichukua. Hamngeweza kumsaidia mchungaji wenu. Ninyi—mchungaji wenu hangekuwa na kazi hiyo kuu akipata mamia mengi ya pesa kwa juma, na kanisa kubwa zuri kuhubiria na kuendesha gari, na kuendelea jinsi wafanyavyo, kama angalilaumu hilo. Dhehebu lingalimtupilia mbali, kwa hivyo lazima yeye alitulize, yampasa alisema. Kwa hivyo yeye ameuzua haki ya mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya mchuzi wa chakula cha dengi ya ulimwengu, ule mchuzi wa Esau. Naye atapata nini badala yake? Wote wawili wataanguka katika shimo la lawama na wahukumiwe. Nawashtaki kwamba wao ni kahaba wa Injili.

228 Nilikuwa kwa kwaya mojawapo wa zile mashuhuri, mahali pakubwa muda mfupi uliopita, kikundu kimoja kikuu sana cha Kipentekoste kilichoko, nami nilikuwa nimeketi katika chumba cha kusomea cha ndugu huyu wakati—kwaya nne au tano zilipokutanika; na ni huko kwa m—moja ya lile—ni kundi moja zuri la madhehebu ya Kipentekoste. Nao hawakujua niko katika chumba cha kusomea cha mhudumu huyu huko Oklahoma. Nami nilikuwa nimeketi chini pale, ambapo mhudumu huyu husomea kabla kuja jukwaani; nami nilipokuwa nimeketi, kulikuwako na hao maskini walaghai wa kiume na wa kike—wamejipaka rangi. Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na nywele ndefu; kila mmoja wao alikuwa na nywele ziliyofupishwa, kila mmoja wao amejirembesha, kila mmoja wao amevaa joho. Na wale wavulana wahuni wakisimama hapo, wakizunguka hivyo. Na mtu fulani alikuwa akichukua sadaka ya umishenari. Yeye alijifanya kama aliye kipofu akiwa na kikombe, na akizunguka-zunguka akinena mambo mengi ya kukufuru kuhusu kuchukua sadaka, na mengineyo; lakini alienda kule na kujaribu kuimba ule—*Yule Masihi* (Jamani!); na wanguimba vema sana, lakini haikutoa ule mlilo wa Kweli. La, kulikuwa kumekufa. Mwaona? Jamani! Ndivyo hivyo. Hiyo ndiyo Golgotha mpya.

229 Waonaje ikiwa msichana au mwanamke fulani mle. . . Kwani kama angeliingia hali amevaa kama impasavyo, akiwa na nywele ndefu, na hiyo rangi ime—imeondoshwa, na mambo kama hayo, wangelimdhiihaki. Kama angalisimama na—wakati yeye alipokuwa akifanya hayo pale. . . Hilo kundi la vijana, wapatao thelathini ama arobaini—kundi lililochaguliwa la Pentekoste na kutenda mambo kama hayo. . . Kama huyo bibi mdogo angenena chochote kulihusu, wangemwondoa katika

kwaya. Hebu mhubiri-Injili asimame mimbarani na anene jambo fulani kulihusu, wangemwondoa dhehebu. Mwasulubisha Mwana wa Mungu upya na kumfedhehi dhahiri. Injili Yake mnayodai mwaihubiri, mmemsulubisha Yeye. Nashtaki hiki kizazi kimkataacho Kristo kwa lile Neno la Mungu, na kwa nguvu Zake za thibitisho hili la siku za mwisho kuwa Yeye yungali hai.

²³⁰ Naam, wanalipinga Neno barabara, lililothibitishwa la Mungu. Madhehebu yao hayawezi kulistahimili.

²³¹ Makanisa makubwa na madhehebu ndiyo Kalvari Yake mpya; nalisema tena. Hawa—wanawake wa kisasa waliovua nguo hadharani ndio kwaya zao. Lo! Makuhani wakuu wa kila dhehebu wanasema kama makuhani wa siku hiyo, “Sasa, shuka na utuonyeshe muujiza.” Hilo lilikuwa ndilo sulubisho la kwanza. Ni hivyo leo. Nimekuwa nao wakisema, “Vema sasa, unawafufua wafu sivyo? Mbona huendi huko? Una mke kaburini; una mtoto huko.”

²³² Wao walimwambia Yeye, “Tulisikia ulifufua wafu. Tuna kiwanja cha makaburi walimojaa. Njoo wafufue...” Jamani, ujinga utazaa ujinga.

²³³ Makanisa makubwa, kwaya kubwa, makuhani wakuu wa siku hizi: “Shuka! utaonyeshe muujiza ambao dhehebu letu haliwezi kuufanya.”

²³⁴ Nilikuwa na mtu fulani, si muda mrefu umepita aliyesema maneno kwenye—baada ya maneno niliyoyasema redioni huko Jonesboro, Arkansas, nikieleza kuhusu kuponywa kwa mwanamke fulani. Mtu huyu alikuwa wa kanisa fulani la kidhehebu, naye akanifuata na kusema, “Namuhimiza mtu yeyote aniletee—anionyeshe muujiza.” Nilikwenda nikampata daktari fulani, mtu fulani alikuwa ameponywa kansa. Nilikwenda nikampata mwanamke aliyekuwa katika kiti cha kusukumia wagonjwa kwa miaka ipitayo ishirini; mwanamke huyo aliponywa ugonjwa wa yabisi kavu, alikuwa katika kiti cha kusukumia wagonjwa. Niliwapeleka huko na kusema, “Sasa, nataka zile pesa, dolla elfu.”

²³⁵ Yeye alisema, “Vema, na... ee... aa... eehe... haziko hapa. Ziko huko Waco, Texas, ndiko makao yetu makuu yaliko.”

²³⁶ Nilisema, “Vema. Tutakwenda huko nikazichukue.” Kasema, nilisema, “Fanya mipango nasi tutakwenda huko kesho.” Mwaona? Nilisema, “Vema tuma...” Nilisema, “Hapa kuna daktari anayesema kuwa watu hawa walikuwa na kansa. Iko hapa kwa orodha ya—picha ya X-ray. Hapa kuna mwanamke huyu ambaye jirani wote wajua yeye aliketi katika kiti cha kusukumia wagonjwa kwa miaka ishirini, na sasa hivi yeye anatembea. Na madaktari... Kumekuwa na daktari baaada ya daktari, baada ya daktari, baada ya daktari, na kadhalika. Na

ndiye huyu hapa mzima leo. Sasa, ulisema ungetoa dolla elfu; nazitaka niziweke kwa hazina ya umishenari. Nazitaka.”

Yeye alisema, “Vema, ziko huko Waco, Texas.”

Nilisema, “Tutakwenda kesho.”

²³⁷ Yeye alisema, “Ngoja kidogo. Hebu nikwambie kitu fulani. Nitamchukua msichana mdogo. Na nichukue wembe na niukate mkono wake, na ndipo umponye mbele ya ndugu zangu; nao watakupa zile pesa.”

Nilisema, “Shetani Wee!”

²³⁸ “Ikiwa wewe u Mwana wa Mungu shuka toka kwa msalabani huu. Twambie ni nani amekupiga.” Hali wamemfunga matambara kukizunguka kichwa Chake, walimpiga Yeye kichwani, kasema, “Sasa, ikiwa wewe u nabii, twambie sasa nani...”

“Ikiwa wewe u Mwana wa Mungu shuka toka msalabani.”

²³⁹ Viongozi vipofu wa vipofu. Wanahitaji kuponywa bongo, mtu awezaye kutenda jambo kama hilo au kunena hivyo. Bila shaka.

²⁴⁰ Ni mlio unaojulikana wa kale ingawaje, “Hebu tukuone ukitenda muujiza. Bwana, twahitaji muujiza kutoka kwako,” wakati kila siku, kila saa ulikuwa ukitendeka kama tu vile Mungu angeongoza itendeke. Lakini wao hawakuwako. Ikiwa walikuwako, wao waliuita Beelzebuli, shetani. Mwaona? “Bwana, tungetaka utende jinsi tutakavyo utenda (ndivyo!), uende tutakapo uende, ufanye tutakavyo!” Lo, naam! Hawakuwa na ushawishi Kwake. La, bwana! Hiyo ndiyo sababu wao walimwondosha kati yao. Naam, bwana! Wao bado wanajaribu kutenda vivyo leo. Na kupitia kwa muungano wa makanisa, mwishowe watafaulu kulitimiza hilo. Wao wote wanaingia; huo ni mlio wa kale unaojulikana.

²⁴¹ Hapa twaona tena mahali pa kidini sana, wanatheologia walio bora na werevu sana, wakitoa wito tena na kumpinga Yeye, wakiita... Wale wanatheologia waliofundishwa vilivyo, wanaopaswa kujua vema zaidi makanisa yaliyo mazuri sana na wanathelologia waliofunzwa vilivyo wamwondosha Yeye kati yao. Hawalitaki. Mwasema, “Hilo ni kosa, Ndugu Branham.” Basi wewe haukuwa hapa kuona *Zile Nyakati za Kanisa* wala kusikiza zikihubiriwa. Hukuwa hapa wakati huu Wakati wa Kanisa la Laodikia ulikuwa ndio pekee ambapo walimtupa Yeye nje ya kanisa; na Yeye alikuwa nje—upande wa nje, akibisha, akijaribu kurudi ndani. Wao walimtupa nje, kwa sababu hawana haja Naye. Wao humsulubisha Yeye upya. Amina! Tungeenda umbali gani?

²⁴² Kumbuka yule nabii wa Neno la Mungu alituambia awali katika 2 Timotheo 3 (ikiwa mnaandika; hatuna wakati wa kukisoma, lakini inasema kuwa) katika siku za mwisho wenye

dhihaka wangekuja. Wangekuwa wakaidi wenye kujivuna, wenye kupenda anasa kuliko kumpenda mungu, wazingiziaji wasiojizua, wakali, na wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi wenye kujivuna, walioelimika, wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake. Hao nao jiepusheni nao, kwa maana katika hao wamo wale wanaowachukua mateke wanawake wajinga, waliofupisha nywele, wanaovaa suruali fupi, wanaopaka nyuso rangi toka mahali pamoja hadi pengine, huwachukua mateka. Ndivyo hivyo hasa. Yeye alisema, Hao nao jiepusheni nao katika siku za mwisho.

²⁴³ Na tumtii nabii. Jiepusheni na mambo hayo katika siku za mwisho. Mko hapa. (Naliambia Kanisa sasa.) Naam, bwana! Jiepusheni nayo.

²⁴⁴ Wao wana—wao... Wa—wahudumu wa siku hizi yawapasa wajue mambo haya. Laiti wangelimjua Yesu katika siku Zake. Iliwapasa kumjua, na sasa inawapasa kumjua; lakini hawamjui.

²⁴⁵ Kama tu vile hao waalimu wa Kiyahudi wa siku Zake walipaswa kumjua Yeye—kwa siku Zake, ndivyo hivyo siku hizi za Neno la Mungu lililothibitishwa dhahiri basi. Yeye alikuwa Neno, na alithibitisha kuwa ndiye Neno. Alithibitisha kuwa Yeye alikuwa Neno la siku hiyo. Na Mungu amethibitisha leo kuwa Yeye ndiye Neno la siku hii, Nuru ya wakati huu. Na iliwapasa kujua wakati huo, na inawapasa wajue leo. Wao walimsulubisha Yeye wakati huo, na wanamsulubisha leo. Nawashtaki kwa ajili ya hilo. Vema. Inazidi tu kuangaza kupitia kwangu. Nawashtaki, kwa sababu Mungu atawaadhibu.

²⁴⁶ Wale Wayahudi wa siku zao... Mungu tena katika siku hizo duniani, Yesu alisema, “Yerusalem, Yerusalem, ni mara ngapi ningekuwa katika kundi moja kubwa mno, lakini hamkutaka.” Jinsi Mungu amejaribu katika siku hizi za mwisho kuwakusanya watu Wake pamoja, lakini hamkutaka. Mmetamani kanuni zenu za imani, basi sasa, mmetolewa kwa maangamizi. Hayo ndiyo Yerusalem ilipokea. Ilimbomolewa, ikateketezwa; haipo tena. Na hivyo ndivyo hasa itakavyokuwa hivi karibuni kwa hivi vitu vikuu hapa. Kanuni zenu kuu za imani na madhehebu yatakufa na kuangamia, lakini Neno la Mungu litakuwa la milele na litaishi daima.

²⁴⁷ Majeraha Yake makubwa sana yalitoka kwa nyumba ya wajiitao marafiki. Waza! Liwazie! Liwazie! Koma! Ninangoja kidogo. Wahudumu, liwazieni! Majeraha Yake yalitoka wapi? Nyumbani mwa wale wanaoitwa marafiki Zake. Kama ilivyokuwa, ndivyo ilivyo. Liwazie! Hapo Kalvari Yeye hakuzungukwa na—na wakatili, washenzi, lakini na wahudumu waliodai wanampenda. Na leo, Injili wakati inatambulikana dhahiri, ishara kuu za kufufuka Kwake zinapothibitishwa kati yetu, si wa barabara ya mji huko wakurukio, ni wale wajiitao wahudumu. Wale wadhaniwao

wampenda Yeye ndio wanaomzingira leo. “Hatutakuwa na kitu hicho kati yetu. Hatumtaki mtu huyu atutawale. Hatutamsaidia; hatutashirikiana na hayo katika mji huu, kitu hicho kikija huku. Si kingine ila kuabudu wafu. Ni shetani.” Kutokujua Neno la Mungu, vipofu wakiongoza vipofu kama ilivyokuwa wakati huo... Waza! Ndivyo ilivyo sasa; kama tu ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa. Waza!

²⁴⁸ Hii nguvu ya kuponya na kuwaweka huru wanaume na wanawake tokana na kupenda ulimwengu huu wa sasa, tokana na kufupisha nywele, Ma-Yezabeli waliopaka nyuso rangi, wanajiita wenyewe Wakristo na kuwa na maisha kama hayo... Wanavuta sigara, wananena mizaha michafu, wanaketi chini na kuunda shirika la kimishenari, na kuunganisha, na kushona, na kuongea, na kukashifu, na—na kutembea—tembea kwenye barabara za mji wakivaa suruali, na kadhalika, na kisha wajiita wenyewe Wakristo mbele ya wanawake wengine.

²⁴⁹ Mwakumbuka hadithi yangu kuhusu yule mtumwa aliyejua kuwa yeye alikuwa mwana wa mfalme, tabia yake. Nasi yatupasa tuweje? Wanaume wa wanawake... Na kukana... hawa makasisi, hii mimbara ambapo Yeye apata michomo Yake, wameanzisha na kuunga mkono aina ya maisha hayo kati ya watu—wakimchoma Yeye. Wao hukana Nguvu ile iwawekayo huru, nao wanaiunga mkono, hali ni kinyume cha Neno la Mungu kwa mwanamke kufupisha nywele zake, au kupaka rangi uso wake, au kuvaa suruali. Ni kinyume cha Neno la Mungu, lakini wao wanayaunga mkono wakitengeneza Kalvari nyingine. Toka wapi? Toka kwa barabara za mji? Toka kilabu cha pombe? Toka mimbarani, toka mimbarani.

²⁵⁰ Na tena, mlio wao ulikuwa nini? “Yeye ajifanya mwenyewe Mungu.” Wao wakana Uungu Wake. Wao hujaribu kumgawanya Yeye na kumfanya Miungu mitatu au minne, hali Yeye yu Mungu. Yeye alikuwa ndiye Mungu. Naye kila mara atakuwa Mungu, Yeye yule jana, leo na hata milele. Unaponena kuhusu Mungu mmoja kwao, wao hukuchekelea. “Twaamini Utatu Mtakatifu.” Namwamini Mungu mmoja mtakatifu, Nguvu Zake za kuponya, kuweka huru, na kuwaondoa watu hawa toka kwa kupenda ulimwengu, kuwaweka huru kama vile Yeye alivyomfanyia Mariamu Magdalena.

Kumbuka, yeye pia alikuwa maskini Yezabeli aliyejipaka rangi.

²⁵¹ Alikuwa na pepo saba ndani yake. Alikuwa mwanamke aliyejivua nguo hadharani, kama tu wanamke wa kisasa barabarani siku hizi. Nenda popote utakapo na utazame. Ikiwa huamini kuwa watu husujudu madhabahuni mwa wanawake walio uchi, tazama barabarani siku hizi. Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa. Tazama kule, usipoliamini. Nenda tu popote. Fungua gazeti la kila siku,

fungua gazeti; tazama matangazo. Unapata nini? Kumbuka yale yaliyosemwa, “Wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu kuwa ni wazuri, walijitwalia wake?”

²⁵² Tazama kashifa za huko Uingereza. Tazama kashifa za hapa. Tazama, jambo lote limekuwa danguro. Mbona hivyo? Mbona Urusi ikawa Ukomunisti? Kwa ajili ya ufidhuli na uovu na kukosa nguvu kwa kanisa Katoliki. Na ndiyo sababu hasa taifa hili linachukua ukomunisti katika muungano wa makanisa na kujiunganisha lenyewe na kanisa Katoliki, hali ukomunisti na Ukatoliki vitaungana pamoja, mwajua. Na hapa wao wanalitenda hilo. Kwa nini? Kwa sababu wao wamekataa Injili inayowatenga wao na kuwafanya watu tofauti. Upuzi! Hiyo hasa ndiyo sababu. Na wahudumu mimbarani wanastahimili hilo kwa ajili ya kujipatia riziki, kwa ajili ya kujisalimisha mbele za kanuni fulani za imani waseme, “Mimi ni mfuasi wa *hiki na kile*,” wakichukua elimu badala ya Nguvu za Mungu.

²⁵³ Waweke huru toka kwa kizazi cha wazimu kama Mariamu Magdalena...Nguvu zile zile ambazo zingemchukua huyo mwanamke uchi barabarani na kumfanya avae nguo, na kutenda kama impasavyo bibi wa heshima, kumfanya awe Mkristo; wao huzilaumu Nguvu hizo na kumsulubisha Mtu aliyekuwa Nazo huko Kalvari.

²⁵⁴ Na siku hizi, Injili ile ile pamoja na huyo Roho Mtakatifu ambayo itamchukua mwanamke aliye uchi hadharani, na kumfanya avae kama mwanamke wa heshima, na kumfanya atende kama Mkristo; wao huiita kurukwa na akili nao hawaitaki ichanganyikane na makutano yao, au ienezwe kati yao na kuwafanya wanawake wengine watende hivyo. Wao wanatendaje? Wanaitupilia mbali kama walivyofanya wakati huo. Na sasa, wao husulubisha Neno lile lile na kusema lilikuwa la wakati mwingine. Nawashtaki tena. Naam, bwana! Vivyo hivyo tu kama walivyoshtakiwa wakati huo.

²⁵⁵ Ile ishara iliyomfanya yule Legioni wa kale avae nguo zake. Mwakumbuka, watu wavuao nguo zao ni wenda wazimu. Mwaona? Na mwanamke, je, Legioni alikuwa wazimu; alivua nguo zake. Mungu alizichukua Nguvu Zake na kumfanya avae nguo zake, akazivaa, ana akili zake, ameketi miguuni pa Yesu. Tazama zile Nguvu zilizomfanya Bartimayo kipofu aone, papo kati ya kanuni zao za imani. Yeye alikuwa duniani wakati kulikuwa na kutokuamini kwingi kama ilivyo siku hizi, lakini hakukumzuia Yeye; aliendelea. Hakuwachezea; Yeye aliwaambia, “Ninyi mu wa baba yenu ibilisi.” Alililaumu jambo hilo lote.

²⁵⁶ Ile Nguvu ambayo ingemfufua Lazaro toka kaburini na kumrudishia yule mwanamke wa Naini mwanawe (ee, Mungu!), ile Nguvu ambayo ingetenda mambo hayo, ambayo ingetabiri mambo yaliyotendeka: “Kuna wana punda wawili—kuna mwana

punda aliyefungwa nje katika njia kuu,” na mambo haya yote ambayo Yeye alitabiri; Mtu yule yule aliyekuwa na Uweza. “Mwondosheni. Hatumtaki kati yetu. Yeye ayachafua mafundisho yetu.” Nao wakamsulubisha.

²⁵⁷ Jambo lile lile siku hizi: “Mwondosheni Roho Mtakatifu.” Hawataki chochote kuhusiana Naye. “Huhukumumu, na kutenda mambo, na kuwaambia watu wetu mambo haya; hatutaki achanganyikane na madhehebu yetu. Anapinga kanuni zetu za imani,” Wao wamsulubisha Yeye tena. Jamani!

²⁵⁸ Tazama sasa, hali tunapomaliza; yatubidi tumalize. Na tena, wao wanaiita kurukwa na akili. Nao walimwita Yeye aliyerukwa na akili. Wao walisema Yeye alikuwa mwenda wazimu. Na kila mtu ajua kuwa Biblia ilisema kuwa Yesu alikuwa—kuwa wao Mafarisayo walisema, “Mtu huyu ni Msamaria, na ni mwenda wazimu.” Sasa, sasa neno *mwenda wazimu* lina maana gani? “mwenye kichaa” “mtu huyo ana kichaa. Ni watu wenda wazimu wanofuatana naye. Yeye ni Beelzebuli.”

²⁵⁹ Na tena, wao husema jambo lile lile: “Ni aina fulani ya uchawi. Ni kupiga ramli.” Wakimwangika Yeye tena msalabani wa aibu. Msalaba gani? Aibu gani? Yeye ni Neno lililothibitishwa, kulifanyia mzaha, kuwaambia watu ni la ibilisi, kufanya kitu fulani. . . kiitwe. . .

²⁶⁰ Yeye alisema, “Wanaziita kazi takatafu za Mungu kuwa zinafanywa na pepo mchafu.” Hakuna msamaha kwa hayo, kulifedhehi Neno Lake, dhahiri, na kuliita uongo au kurukwa na akili.

²⁶¹ “Usiliendee. Usihudhurie mikutano hiyo.” Je, wao hufanyaje kwa kutenda hilo? Huchukua misumari ya kanuni za imani zao za kidhehebu. Hiyo ni kweli. Hawa waalimu watafuta-anasa, wa kilimwengu, wasiomcha Mungu, wazimu wa kidhehebu, huchukua misumari ya kidhehebu na kumsulubisha Mwana wa Mungu nayo upya toka mimbarani. Mbona wao hutenda hili? Wao hupenda sifa za wanadamu, zile shahada ambazo kanisa huwapa, kuliko kupenda Neno la Mungu. Nawahukumumu. Hawawezi kuifuatisha namna ya dunia, kwa sababu wao wana—hawawezi kupatana na Neno, kwa sababu wao wamekwisha patana na ulimwengu. Tayari wao wame. . . Hi—hizi ni siku za kinafiki tunazoishi!

²⁶² Je, hii—Kalvari moja haitoshi kwa Bwana wangu? Mbona mwatenda hivi? Ninyi mnaodhaniwa mwampenda Yeye, ninyi mnaojua hili ni lile Neno Lake, ninyi mwezao kusoma Ufunuo sura ya 22 na kusema, “Mtu ye yote akiondoa neno moja au akiongeza neno moja,” mbona mwa fanya hivyo? Je, si Kalvari moja yamtosha Yeye? Niko hapa kumtetea. Mimi ni wakili Wake. Nami nawashtaki kwa Neno la Mungu. Badilisheni njia zenu, la sivyo, mtatokomea kuzimuni; madhehebu yenu yatavurugika. Nawashtaki ninyi mbele ya Hakimu. Bila shaka. Ninyi, wenye

mfano wa utauwa, unafiki. Mwauita nini? Je, Kalvari moja haitoshi?

²⁶³ Kama Petro alivyosema, “Baba zenu wa kidhehebu...” Petro aliwashtaki ninyi kwa... alisema, “Ni nani kati ya baba zenu hakutenda hili?” Stefano alifanya vivyo hivyo. “Kwa mikono ya watu wabaya mmemsulubisha Mkuu wa Uzima.”

²⁶⁴ Je, si Yesu Mwenyewe alisema, “Ni nani kati ya baba zenu hakuwaweka manabii kaburini? Nanyi mkayapamba baadaye?” Ndivyo imekuwa kwa watu wenye haki katika nyakati zote. Ndivyo nawashtaki hawa watu wakuu, walioerevuka, kundi la waenda-kanisani wakataa-Kristo wa siku hizi. Ninyi na mifano yenu ya utauwa mwamsulubisha Kristo wangu mara ya pili kwa kuwaambia watu kuwa maneno haya ni ya wakati mwingine, na si ya wakati huu. Nawashtaki ninyi. Mna hatia ya uasi ule ule waliokuwa nao siku waliyomsulubisha. Tubuni mkamumrudie Mungu au muangamie! Na tena nasema, *Hapa*, makanisa; *wao*, waalimu; *wanamsulubisha*, kwa kukufuru: *Yeye*, Neno. Mungu uturehemu! Hebu na niseme hilo tena; huenda imechanganyikana kwa kanda. *Hapa*, makanisani; *wao* wahubiri; *wanamsulubisha*, kwa kukufuru; *Yeye*, Neno. Si ajabu tena ni,

Miongoni mwa miamba inayopasuka na anga
zenye kiza

Mwokozi wangu alikiinamisha kichwa Chake
akafa.

Lakini pazia iliyofunguka ilifunua njia

Kwenda rahani za Mbinguni na siku isiyo na
mwisho.

²⁶⁵ Nayasema kwa kanda hii na kwa wasikizaji hawa; nasema hili chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, “Ni nani aliye upande wa Bwana? Na aje chini ya Neno hili.” Hakika Mungu ataleta hiki kizazi kiovu, kikataa-Kristo, kikana-Kristo hukumuni kwa kukufuru, kule kusulubishwa kwa Neno Lake lililothibitishwa. Mnakuja hukumuni. Nakishtaki! “Ni nani aliye upande wa bwana?” Musa aliuliza, “Na aje kwangu,” hali ile Nguzo ya Moto ikining’inia hapo kama ushahidi. Ni nani aliye upande wa Bwana? Na alichukue Neno na akane kanuni zake za imani, na amfuate Yesu Kristo kila siku. Nami nitakutana nawe asubuhi ile.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi.

²⁶⁶ Ee, Bwana Mungu, mpaji wa Uzima wa milele na uli—uliye Mwandishi wa hili Neno, uliyemfufua tena toka kwa wafu Bwana, Yesu. Yule aliyethibitishwa vema mbele ya—ya kizazi cha watu wasioamini; imekuwa muda mrefu sasa asubuhi hii. Wengi wameketi hapa (kanisa limejaa), watu wamesimama kote ukutani, na kanda zinatengenezwa ziende ulimwenguni kote, mahali mbalimbali. Wahudumu watasikia hili katika mahali pao

pa kusomea. Nawaombea, Bwana. Na haya maneno yaingie sana moyoni, yapenye sana, yaondoe Ulimwengu wote, ili wao waweze kusema, kama mhudumu huyu wa Kimethodisti huko Kentucky alivyonijia siku moja na kusema, “Nilipokuwa nikisikia hizo *Nyakati Saba Za Kanisa*, nilisikia ikilia, ‘Ondoka kwenye kuta za Babiloni!’” Kasema, “Nililiacha na kuondoka. Sijui niende njia ipi au nitende nini, lakini niliondoka.” Na ubarikiwe ujasiri wa kijana huyu mwenye mke na watoto wawili au watatu.

²⁶⁷ Mungu, na wengi wapate njia yao kuelekea kwa Neno la Mungu, njia pekee ya Uzima, maana Yeye ndiye Neno. Namwombea kila mmoja, Baba. Wakati mwingine kwa kusema mambo haya, si kwa ukali, ni kwa upendo; maana upendo husahihisha makosa. Nami naomba, Mungu, kuwa watu wataifahamu hiyo; kwamba imekusudiwa kuwa sahihisho.

²⁶⁸ Wewe uliyepaswa kuwasahihisha, uliwaombea msalabani ukisema, “Baba wasamehe. Wao—wao ni vipofu; wao—wao hawajui watendalo.” Nawaombea wahudumu wa siku hizi wanaolisulubisha lile Neno tena kwa kuchukua kanuni za imani zao, na madhehebu na mafundisho ya sharti, na kubadilisha hayo na Neno la Uzima. Na ndipo, mbele ya watu wao—wao hulaumu ile Kweli halisi ambayo Mungu anathibitisha kuwa Kweli Yake. Twawaombea, Baba, kuwa utawaalika tena kwa Karamu ya Arusi. Na wao waje wakati huu bila udhuru, maana natambua huenda mwaliko wa mwisho umekwisha kutolewa. Huenda kumechelewa sana sasa. Natumai siyo.

²⁶⁹ Na bariiki hawa makutano wachache walio hapa, hawa watu mamia machache waliokusanyika ndani humu asubuhi hii, siku hii yenye joto jingi, wameketi hapa kwa muda, labda masaa mawili au zaidi ya ibada wakisikiza. Hawajaondoka; walitulia tu na kusikiza. Wengi wao wakingoja chakula chao cha kutwa, na wanawake wakisimama pamoja na watoto wao wachanga, nao wanangoja. Wanashikilia kila Neno.

²⁷⁰ Bwana, natambua kile kitakachotendeka kwangu siku ya hukumu ikiwa niliwaongoza watu vibaya. Ninafahamu, Bwana, niwezavyo kujusikia, kuwa najaribu kuwapeleka kwa Neno, wapate kuishi kwa Neno nikiwaambia wao Wewe ndiwe yule jana, leo na hata milele, na kwamba Roho Mtakatifu mkuu ni Yesu Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu, Mtu yule yule. Wewe ulisema hivyo. “Kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mtaniona Mimi, maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Nami najua kuwa huyu Ndiwe, Bwana, nasi twakuamini Wewe, maana twakuona ukitenda jambo lile lile kati yetu.

²⁷¹ Twajitolea wenyewe kama—leo, kwa utulivu; twafanya hivyo hapa katika makutano haya. Na kwenye kanda, Bwana, kwa wakati huu, na kila mwanamume na mwanamke, na mvulana au msichana aliy—aliyekoko hapa, au amesimama nje, au anayesikiza

kanda, na sisi kwa wakati huu tujiweke wakf sana na tujitolee nafsi zetu zote kwa utumishi wa Mungu.

²⁷² Tembea kati ya wasikilizaji hawa, Bwana, katika nguvu na uponye wagonjwa. Wao walisema wana mvulana mmoja aliye kiwete anayeketi upande huu hapa. Na huyo Roho Mtakatifu mkuu... Twajua kuketi tu Uweponi Mwake kama hivi ni... Atalitekeleza. Kama ungeweza kupitia redioni na televisheni, nje kote nchini na kuponya wangojwa (Wewe ulituma Neno Lako na liliwaponya), Wewe waweza kutenda jambo lile lile dakika hii. Naomba, Mungu, kuwa utamponya kila mtu aliye mgonjwa, kila kiwete, kila anayeteseka hapa na wale wasikiao maneno haya. Mungu, tujalie. Ombi langu ni juu yao. Pamoja na—pamoja na upendo wa Kristo moyoni mwangu na kuhuzunikia wenye mahitaji, nawatoa wao, Bwana, Kwako juu ya madhabahu ya dhabihu, ambapo ule mwili uliojawa damu wa huyo Mwana-Kondoo umewekwa kama kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu na magonjwa, umewekwa hapo. Naomba neema kwa ajili ya watu hawa. Nataka nisimame kama Musa alivyofanya pengoni kwa ajili yao, Bwana, na kusema, “Mungu, uwarehemu—warehemu kwa muda mwingine zaidi na uwape nafasi nyingine.” Usi—Usilifanye sasa hivi Bwana. Ruhusu—iruhusu Injili ienee mbali kidogo tena.

²⁷³ Wao—wao wamehukumika, Bwana. Naomba kuwa huruma zako kuu na neema zita—zitaenezwa hata kwa mtu wa mwisho ambaye jina lake liko kwenye kile Kitabu. Nami najua wata... Si vigumu kuomba dhidi ya Neno Lako la Kiungu—dhidi—au dhidi—ukiwa na Neno la Kiungu, nakusudia kusema, Bwana, Neno lililoahidiwa, Neno ambalo limethibitishwa, na Neno ambalo liliwachagua watu hawa tangu asili huko nyuma kabla dunia kuwekwa misingi. Si—si vigumu ku—kuomba kuwa Wewe utawaokoa ambao majina yao yamo mle Kitabuni, maana najua Wewe utalitenda; Yesu alisema hivyo; “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Na hakuna awezaye kuja asipotolewa.

²⁷⁴ Sasa, naomba, Mungu, kuwa kila mahali maneno haya yaangukapo, kwa kanda na pia kwa wale walio hapa, kuwa Roho Mtakatifu atamwita kila mtu aliyechaguliwa asili hivi sasa, tangu dunia kuwekwa misingi wakati majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Na wasikie sauti ya Mungu ikinena leo, na hiyo Sauti ndogo, tulivu na nyembamba mioyoni mwao ikisema, “Njia ni hii, ifuateni.” Tujalie Baba. Naomba katika Jina la Yesu.

²⁷⁵ Na hali tukiwa hapa sasa, vichwa vyetu vimeinamishwa hapa katika wasikizi, mwaamini hii kuwa Kweli, na ninyi—ninyi... (Naweka—naweka mkono wangu juu ya vitambaa hivi vilivyowekwa hapa na vifurushi vya wagonjwa na wenye dhiki.) Nataka kuwauliza swali, kwa moyo mweupe sasa. Siji hapa tu nisikizwe. Ni—ni—nimechoka; nimedhoofika. Mimi si kijana kama nilivyokuwa, na ni—nami najua siku zetu

zimehesabiwa. Nami najua napaswa kuingiza kila kitu kidogo niwezacho kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Yanibidi kuhubiri kila wakati niwezapo kupata nafasi. yanibidi niende—Yanibidi niende nikitaka au nisipotaka. Mimi huja hapa kwa sababu na—najisikia kufanya hivyo; ni—nataka kufanya hivyo. Nami nawapenda ninyi. Nami sisemi mambo kwa ukali na uzito kwa—kwa—sababu nataka kusema hivyo; kuna—kuna kupuma ndani yangu. Jambo lile lile ambalo limethibitishwa ndilo linifanyalo nitende mambo haya. Nami nasema kwa upole, kwa upendo. Sikusudii kuwakaripia wanawake wetu au wanaume wetu. Sikusudii kufanya hivyo, ndugu, dada; nakusudia tu kuwaleta ninyi hadi ma—mahali palipochongoka ambapo mwaweza kuona sahihisho na ule mjeledi wa Bwana, ili iw lazimu kuingia sasa. Usiliahirishe sasa; huenda ukangoja zaidi sana.

²⁷⁶ Nanyi mnaotamani kuja upande wa Bwana pamoja na kujitolea kwa mioyo yenu yote mbele za wasikilizaji sasa, au huko katika nchi ambamo kanda hii itakuwa, ninyi, vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa... Msiinue mikono yenu ikiwa hamukusudii hivyo. Sasa, ikiwa unakusudia kabisa kwa Bwana pamoja na maisha yaliyotakaswa sana, nakutaka uuinue mkono wako hivi sasa. Wewe... Bwana akubariki. Unajitakasa mwenyewe upya kwa Kristo kwa kujaribu kuchukua ile shutuma. Sema, “Ninataka leo kuchukua shutuma hiyo.” Mimi pia nimeiinua mikono yangu yote miwili. “Nataka kuchukua ile shtuma ya Yesu Kristo juu yangu. Kwa furaha naivaa hii alama itwayo ‘watakatifu wanaojigaragaza’ au vyo vyote utakavyotaka kuiita. Naivaa kwa ujasiri, kwa sababu ni kwa ajili ya Bwana. Naivaa kwa ujasiri.” Je, ninyi nyote hamtaki kufanya vivyo hivyo? Inueni mikono yenu na mkaseme, “Kwa neema ya Mungu, ni—ni—nataka...mimi...”

²⁷⁷ Wale wanafunzi waliporudi, walifikiri lilikuwa jambo la heshima kuu kuchukua shutumu ya Jina Lake. Au wataka kuchukua shutumu ya mchezaji fulani wa Hollywood, au kitu fulani cha televisheni, au mwanachama fulani wa kanisa, au mwingine yule, au, je, wataka shutumu ya Neno la Yesu Kristo? “Nipe mimi shutumu ya Neno, Bwana. Najua Yeye aliichukua aibu ya Neno, Bwana. Hebu nami niichukue pia, Bwana.

Na huu msalaba uliowekwa wakfu nitaubeba,
Hadi kifo kiniweke huru,
Ndipo niende nyumbani, nikavikwe taji. . .”

²⁷⁸ Siku moja kutakuwako na taji kwa ajili yetu. Inatengenezwa sasa. Haya maisha ya duniani yaishapo, ndipo tutajua ni kweli.

²⁷⁹ Sasa, hakuna nafasi kuwaleta watu madhabahuni. Basi viti vyenu mlipo viwe madhabahu. “Na wote waaminio...” Tunapoomba.

²⁸⁰ Baba aliye Mbinguni, yaonekana kama mikono mingi ya vijana na wazee ilikuwa juu katika wasikilizaji hawa. Nami

naomba kuwa kila wakati kanda hii itakapochezwa watu wataweka mikono yao juu na kupiga magoti chumbani. Baba na mama, waende wakishikana mikono mmoja kwa mwingine na kusema, “Mpenzi, tumekuwa washiriki wa kanisa muda mwingi kutosha. Na tumjije Kristo.” Tujalie, Bwana.

²⁸¹ Wabariki watu hawa hapa. Naomba kuwa utawapa, Bwana, maisha matakatifu. Wengi wao, Bwana, ni watu wazuri. Wao ni watu Wako; wao hawajajua ile Kweli. Nami naomba kuwa Wewe utawaonyesha Kweli Yako, Bwana, “Neno Lako ni Kweli.”

²⁸² Kama ulivyosema katika Yohana, nadhani labda sura ya 17, wewe ulisema, “Uwatakase, Baba, kwa ile Kweli. Neno Lako ni Kweli.” Na hilo—tena, Neno Lako bado ni Kweli. Kila mara ni Kweli, kwa sababu ndilo Mungu. Nami naomba, Mungu, kuwa utawatakasa kwa ile Kweli; yaani, watakase, waoshe, wawe safi toka kwa kanuni zote za imani na madhehebu; wasafishe toka kwa mambo yote ya kilimwengu hadi kwa maisha yaliyowekwa wakf ya lile Neno. Tujalie, Bwana. Wao ni wako sasa; Wewe uliahidi kulitenda hivyo. Na kama mtumishi Wako, naomba dua yangu kwa niaba yao. Katika Jina la Yesu Kristo.

²⁸³ Sasa, vichwa vyetu vikiwa vimeinamwishwa, na tuuimbe wimbo huu hali tukiendelea kuomba.

Deni ya dhambi,
Msalabani (wazia hilo!)
Ilimalizikia,
Ni huru kabisa.

²⁸⁴ Jana nilikuwa mahali fu—fulani, na mtu fulani alikuwa akinipima suti ambayo ndugu fulani hapa kanisani alininunulia. Yeye alisema, “Suti yako ilionekana joto, nami nilikununulia ya baridi kidogo.”

²⁸⁵ Nami nilikwenda kuipima, naye alisema, “Aisee, bega lako la kulia lainama chini. Lazima wewe ulibeba mzigo mzito wakati fulani.”

²⁸⁶ Nami niliwaza, “Naam, mzigo wa dhambi, lakini Yesu alilipia wote.” Sikiza tunapouimba.

Deni ya dhambi.
Basi m—(maisha yangu yote) salabani,
(Dhambi ilifanyaje?)
Ilimalizikia,
Ni huru kabisa!

²⁸⁷ Mungu, turehemu sisi kama huu wakati mkuu wa kumwazia Mungu. Na Neno likolee sana, Bwana, mioyoni. Na watu, ingawa wamechelewa kula chakula chao cha kutwa, bali, Bwana, hili ni zaidi ya chakula; hili ni Uzima. “Neno Langu ni chakula,” Wewe ulisema. Na hilo ndilo nafsi zetu zenye njaa zinakula.

²⁸⁸ Sasa, tuchukue, Bwana, utufinyange; Bwana, unichukue pamoja nao. Nataka kwenda pamoja nao. Ninakwenda hadi

Kalvari sasa. Bwana kwa imani. Nakwenda pamoja na hawa makutano. Sasa, nifinyange tu tena, Bwana. Nimetenda makosa. Mara nyingi nime. . . Hapa hivi majuzi, nilitaka kuacha kuhubiri. Watu hawangenisikiza. Wao walizidi tu kutenda jambo lile lile, nami—na nilishushwa moyo. Nilishikwa na kinyongo. Ee, Mungu, Jumapili chache zilizopita uliponipa ishara hiyo huko nje, na si—na nikisoma Biblia na kuona kuwa ulimwambia Musa, kama tu vile hiyo ndoto ilivyokuwa, kuwa palikuwapo mlima pia ambao ungekuwa ishara kwake. Na ndipo mwishoni mwake kabisa kujua kuwa ninge—nginewaacha watu wengi walio wagonjwa, huduma isiyo tu ya kiunabii, bali pia ya kufundisha lile Neno na—na kwa ajili—kuombea wagonjwa. Wewe ulimwachilia mtu aanguke papa hapa sakafuni akafa, ndipo ukamfufua tena kuthibitisha kuwa ilikuwa kweli. Wewe kila mara huthibitisha Neno Lako.

²⁸⁹ Sasa, Bwana, lithibitishe hivi sasa hali niko mbele ya Kiti Chako cha Enzi. Chukua kila mmoja wa watu hawa, Bwana, ondoshwa ulimwengu ndani yetu. Nitwae, Bwana, tungali katika uwepo Wako. Chukua tu lile Neno; kamua moyo yetu. Mungu, sasa hivi, ondoa ulimwengu na shughuli za ulimwengu mbali nasi. Na tuwe Wakristo waliotakasika, ee, Mungu, tuwa wapendao, na wakarimu, na wazuri, tukizaa lile tunda la Roho. Je, utalitimiza, Bwana? Tuko mbele ya kiti Chako cha Enzi. Dhambi imeacha alama nyekundu juu ya kila mmoja wetu, lakini Damu Yako yaweza kuiondoshwa, Bwana, na kuisafisha iwe nyeupe kama theluji. Tujalie tungali tukikungoja Wewe. Tutwae; sisi tu Wako. Twaweka wakfu maisha yetu Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo. Tujalie, Bwana, kila mmoja wetu.

²⁹⁰ Kamua moyo wangu, Bwana. Naziona kasoro zangu zote; naona makosa yangu. Mungu, tangu sasa ninajaribu kuishi vema niwezavyo kukusaidia Wewe. Nataka kwenda—nataka kutakasa maisha yangu upya Kwako hapa asubuhi hii. Baada ya kulileta shtaka hili dhidi ya marafiki wa—wangu wahubiri huko, na yanibidi niseme mambo haya magumu; lakini Bwana, niliyatenda kwa punzi Yako. Najisikia kuwa Wewe uliniambia nitende hili. Sasa, haumo mabegani mwangu, Bwana. Ni—ninafuraha umeniondokea. Na wao watende nao lo lote wapendalo, Baba. Naomba kuwa wataupokea.

²⁹¹ Naomba kuwa Wewe utamwoko kila mmoja, Bwana. Na humo kutokee ufufuo wa wenye haki na Uweza mkuu uje kati ya Kanisa kabla tu ya kuondoka Kwake. Si vigumu kuomba hayo, kwa maana Wewe uliyaahidi.

²⁹² Nasi twatazamia, Bwana, huo mvuto wa tatu tunaojua kuwa utatenda mambo kati yetu.

²⁹³ Mimi ni Wako, Bwana. Najilaza mwenyewe kwenye madhabahu haya, kwa kujitakasa kama tu ni juavyo kujitendea mwenyewe. Ondosha ulimwengu ndani yangu, Bwana. Yaondoe

mambo yaharibikayo kwangu; nipe mambo yasiyoharibika: Neno la Mungu. Na niweze kuishi karibu sana na hilo Neno, hata lile Neno liwe ndani yangu na mimi ndani yake. Nijalie, Bwana. Nisiondoke kwalo kamwe. Nikashikilie kwa nguvu ule Upanga wa Mfalme na kuunyaka sana. Nijalie Bwana.

²⁹⁴ Tubariki sote pamoja. Sisi ni watumishi Wako, tunapojiweka wakfu Kwako asubuhi hii, upya, mioyoni mwetu. Sisi ni Wako katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili utumishi.

Deni ya dhambi, (Mungu awabariki! Ndugu
Neville.)

Msalabani,
Ilimalizikia,
Ni huru kabisa.



LILE SHTAKA SWA63-0707M

(The Indictment)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Julai 7, 1963, kwenye Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2011 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org